

Reidun Aambø

Je, kukosa nidhamu ni kawaida kwa Wanorwe?

Typisk norsk å være uhøflig?



Reidun Aambø

Je, kukosa nidhamu ni kawaida kwa Wanorwe?

Typisk norsk å være uhøflig?



HØGSKULEN I VOLDA



MØREFORSKING

2010

Author	Reidun Aambø
Translator	Joseph Akonga
Publisher	Volda University College
ISBN	978-82-7661-289-9
Type set	Joseph Akonga / Bente Lien
Illustration	From the book <i>Is Rudeness Typically Norwegian?</i> , illustrated by Akin Düzakin.
Distribution	Fagbok Volda e-mail: fagbok@hivolda.no tel.: 70 07 53 85

JE, KUKOSA NIDHAMU NI KAWAIDA KWA WANORWE?

Utangulizi	5
Hadithi mbili zilinipa wazo la kuandika kitabu hiki	7
Nidhamu – kutoka kasrini hadi kibandani.....	8
Nidhamu inazungumzia matarajio, wala sio kuwa au kutokuwa sahihi.....	9
Kwa nini tunataka kuwa na nidhamu?.....	9
Je, Wanorwe wanaweza kukosa kanuni za kirasmi, ilihali wawe na nidhamu kwa wakati mmoja?	10
Tamaduni ”moto” na ”baridi”	13
Maneno madogo ya heshima – je, ni maneno yasiyo na maana, njia ya kujigamba, au njia ya kuwa na nidhamu?	14
<i>”Kumaanisha kwa kweli”?</i>	14
Ni rahisi mno kugundua mizigo yako ya kitamaduni unapokutana na wageni	16
<i>Ni njia ipi bora ya kusema hapana?</i>	17
<i>Njia ya kinorwe ya kuwa na nidhamu yaweza kupokelewa na watu wengine kama ukosefu wa nidhamu</i>	18
Wanafunzi wa kigeni na wakaaji wa Norwe kutoka nchi zingine wanaisifia sana njia ambayo wanorwe wanajitaadabu.....	21
Ile hali ya kuzihukumu tamaduni na mazoea ya kinorwe inategemea macho yanayotazama	26
Ni vigumu kukosa nidhama kwa ”njia sahihi”	30
<i>”Wageni wenye tabia mbovu”</i>	30
Hali ya kuwa na imani na watu	33

Utangulizi

Kitabu hiki kina maandishi ya kiswahili na kinorwe. Wazo limekuwa kufafanua kwa njia bora zaidi kanuni za nidhamu za kinorwe – kama zinavyotumika kati ya marafiki na majirani, maisha katika jamii, kazini na katika safari.

Kikundi kinacholengwa haswa ni wageni waliokuja Norwe kusoma, kufanya kazi, au kama wageni tu. Maandishi haya pia yatasaidia sana wale wanaojifunza kinorwe kama lugha ya kigeni. Wasomaji wanorwe wataweza kupata fahamu kuhusu jinsi utamaduni wa kinorwe na njia za kujitaadabu zinaonekana na kueleweka na wageni, kwa kuwa maandishi yana mifano mingi ya jinsi wanafunzi wa kigeni na wakaaji wa kigeni wanavyowatazama Wanorwe walio Norwe na ng'ambo. Maoni yao yameongezewa pia na maarifa ya mwandishi yanayotokana na kusoma, kufanya kazi, na kusafiri katika nchi zinigine. Ni matarajio yangu kuwa utafurahia kitabu hiki!

Natoa shukrani kubwa kwa mwenzangu Humphrey Joseph Akong'a wa Chuo Kikuu Cha Volda, Norwe, kwa kutafsiri katika lugha ya kiswahili.

Volda, Januari 2010

Reidun Aambø

Hadithi mbili zilinipa wazo la kuandika kitabu hiki

Miaka michache iliyopita, mwanafunzi mwethiopia katika Chuo Kikuu Cha Volda aliandika insha kuhusu msaada unaopatiwa nchi yake kutoka Norwe, na akaandika yafuatayo katika kitabu kizee cha wageni katika kituo cha kimishonari: ”Mwanamume mwenye rangi pinki kutoka Norwe alikuja kututembelea jana. Alizunguka akitubughudhu sisi sote.”

Mwanafunzi kutoka Mongolia alieleza hadithi ifuatayo kutoka mji anakotoka, Ulan Bator: ”Ili wakutane na wenyeji huku, wafanyikazi wa misaada ya dharura kutoka Norwe waliwaalika watu wote kwenye karamu, na watu wengi walikuja, vijana kwa wazee. Tulikula chakula na kufurahi. Ilipokaribia mwisho wa karamu, Wanorwe walipatia familia zote zawadi: kijisaduku la huduma ya kwanaza kutoka Red Cross iliyokuwa na mipakato, tambaa, chachi na vifaa vingine vya kimatibabu. Wamongolia waliwashukuru Wanorwe na kuenda nyumbani. Walikuwa wamepigwa na butwaa – na wamekasirika. Sisi vijana hatukukubaliwa kujihusisha na maandalizi yoyote zaidi ya kikundi kile, na watu waliendelea kuongea juu ya kisa hicho miaka mingi mbeleni.”

Ni kipi kiliwaendea mrama wale Wanorwe waliokuwa Uhabeshi na Mongolia? Hakuna anayejua kwa hakika jambo ambalo ”mwanamume pinki” kutoka Norwe alisema na kufanya katika kituo cha kimishonari kule Uhabeshi. Labda alionyesha nidhamu katika njia ya kinorwe kwa kuwaamkia wanaume na wanawake kwa njia sawa, labda bila ya kufikiria cheo, umri au kanuni. Bila shaka alijaribu kusema jambo zuri, labda alingusa mtoto kichwani kama ishara ya urafiki. Na wafanyikaza Wanorwe kule Mongolia walitaka kupatia kila familia zawadi yenye manufaa, kitu ambacho wangeweza kutumia, na walichagua zawadi kwa njia iliyokuwa bora zaidi kwa maoni yao. Lakini zawadi zinaweza kuwa na maana ya kisiri. Wazo linalofuata lilikuwa kwa kweli jipya kwa hao Wanorwe waliokuwa na kusudi zuri: mipakato na tambaa kama zawadi ilimaanisha kuwa waliwatakia Wamongolia siku za usoni zilizojazwa na ugonjwa na matukio mabaya.

Labda tunaweza kusema kuwa ikiwa Wanorwe watabaki Norwe, hawatawahi kutoeleweka kama wenzao kule Uhabeshi na Mongolia. Hadi miaka ya 1970 katika nchi ya Norwe, tunaweza kuzungumzia utamaduni wa kijumla ambapo watu walikuwa na hali sawa ya elimu, dini sawa, vipeo sawa na kanuni sawa. Tulisikiliza vipindi sawa kwenye redio, tulisherehekea sikukuu sawa na tulienda likizoni na kufanya kazi katika nchi yetu. Siku hizi Wanorwe wanasafiri sana na mbali, katika likizo, katika kazi na katika safari za kielimu. Kuwa Mnorwe leo haimaanisha kama vile ilivyomaanisha katika miaka ya 1970. Katika miaka hiyo, idadi kubwa ya watu ilikuwa Wanorwe halisi na wafanyikazi wageni kutoka Pakistani. Katika mwaka wa 2007, tunaweza kupata zaidi ya nchi 200, na tamaduni na lugha nyingi zaidi katika mipaka ya Norwe.

Katika nyakati zilizopita, ilikuwa labda kweli kusema kuwa Wanorwe walikuwa na nidhamu iliyowatosheleza kuishi katika jamii iliyokuwa na mchanganyiko mdogo wa kitamaduni. Kile ambacho sisi katika nchi ya Norwe tunaita nidhamu hakiwezi kutajwa bila ya migongano. Katika jamii ya mchanganyiko, kuna hatari ya kutoelewa wengine na kutoeleweka

mwenyewe, kwa sababu watu wana kanuni tofauti tunapozungumzia nidhamu na tamaduni za kuishi katika jamii.

Nidhamu – kutoka kasrini hadi kibandani

Kulingana na Falk & Torp katika kitabu chao *Etymologisk ordbok* (1992), neno *nidhamu* lina uhusiano na maneno mazee ya kijeremani kama *høvelik* na *höflich*. Lugha ya kinorwe pia imehifadhi *høvisk* (na *det som høver seg*) ambayo yamekopwa kutoka eneo la kati kule Ujeremani *hovesch*. Katika lugha zee la kinorwe, tunapata neno *kurteiss* ambalo lina uhusiano na maneno ya kifaransa *courtois*, *la courtoisie* (yaani, njia fulani za kujitaadhabu katika nyumba ya mfalme, *à la cour*). Katika maneno mengine, nidhamu ni kitu kifalme, kinachojengwa, chenye upole, chenye mafunzo, chenye ustaarabu na alama ya malezi mema.

Ni wachache mno ambao wanaweza kudai kukwa Wanorwe ni wenye nidhamu, haswa kwa kuonyesha tabia za kirasmi na kuonyesha kauli tofauti zinazoafikiana na kila sherehe. Wanorwe wenyewe wanajua kuwa Waswidi wana nidhamu zaidi ya wao. Wenye nidhamu zaidi, wenye kufana zaidi, na wenye madhubuti zaidi, wengine huongezea. Kama tutalinganisha nchi mbili zenye tamaduni zinazofanana kama Norwe na Swidi, itaonekana jambo la jawabu kudhani kuwa Waswidi wana mifano bora zaidi ya nidhami ambayo imetiwa nguvu zaidi na utawala thabiti wa kifalme, vibwana vya kifaransa, vibwana ambavyo vilileta ladha zao binafsi na njia zao za kujitaadhabu kutoka kwa makasri kule Ufaransa. Ni dhahiri shahiri kuwa kukutana na tamaduni geni, historia ya nyumbani na ya kigeni pamoja na majukumu ya kijinsia, hali ya maisha, namna za kutafuta riziki, pamoja na njia za kuonyesha nidhamu, zote zinachangia katika kutengeneza tamaduni za kuonyesha nidhamu katika jamii fulani. Lakini njia hizi hubadilika kila wakati.

Hali ya kuwa na nidhamu inaonelewa kuwa jambo zuri. Nidhamu huonekana katika njia zetu za mazungumzo, na katika njia zetu za kujitaadhabu. Lakini nidhamu pia yaweza kumaanishi kutosema au kutofanya jambo fulani. Na kile ambacho kinaonelewa kuwa cha nidhamu, chenye mafunzo, chenye malezi mema na chenye kukubalika, kinatofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine.

Kila hali inahitaji kanuni tofauti. Tuna kanuni za kuamkuana, za kutembeleana, za kula na wakati wa kula, za kupeana na kupokea zawadi, na kadhalika. Tunachagua kanuni tofauti za kujitaadhabu na njia za kuwasiliana kulingana na kama tuko kwenye jumba la densi, kwenye darasa, au kwenye ibada ya mazishi. Tunatumia njia tofauti za kujitaadhabu na kauli tofauti pia katika familia na kazini ili tuonyeshe kuwa sisi ni wenye nidhamu, na kuwa sisi ni rafiki. Tuanaathirika pia tunapozungumza na marafiki au wageni, na mambo kama jinsia, umri na cheo yanachangia katika viwango tofauti.

Kwa hivyo tunachagu maneno na njia za mawasiliano kulingana na hali, mtu ambaye tunawasiliana naye, jambo tunalozungumzia na hali yetu sisi binafsi. Tunafanya haya yote bila kufikiria tunapotumia lugha ya mama na tulipo katika nchi zetu, lakini katika tamaduni geni tunakumbwa na ugumu wa kutumia kanuni na makonyezo sahihi. Lugha ya kimwili na makonyezo ya uso zina uhusiano na nidhamu na ukosefu wa nidhamu na zinaweza kutafsiriwa kwa njia tofauti. Muda tunaotumia kumtazama mtu, eneo la mwili wake ambalo

tunatazama, ishara tunayofanya na mikono, mdomo na pua na kadhalika, zinaweza kuwatumia watu habari fulani. Hatuzaliwi na njia hizi za kuonyesha nidhamu, lakini twajifunza kama gawo la utamaduni tunaolelewa nao. Kwa kawaida, kanuni hizi hazijaandikwa, wala hazisemwi waziwazi. Ni kanuni hizi tofauti ambazo zinatufanya tuhisi kwamba tumekosea au tujipate tunasitasita, na kutupatia hisia za kutokaribishwa. Ikiwa utatoelewa kanuni hizi, itaathiri kiwango ambacho utaelewa na utahisi kuwa kuna kuvunjika kwa mawasiliano.

Nidhamu inazungumzia matarajio, wala sio kuwa au kutokuwa sahihi

Utamaduni wetu unatufunza tuwe na nidhamu. Ni jambo la kawaida kuwa kila mtu anakusudia kuona ishara zile zile za kuonyesha nidhamu na urafiki zinazopatikana katika utamaduni wake, kwa sababu twazifahamu ishara hizi vyema. Tunapokosa kuona ishara hizi tunapozitembelea nchi geni, ni rahisi kudhani kuwa watu huko wana ukosefu wa nidhamu. Kuelewa kile ambacho kinaonyesha nidhamu inahusu kutosheleza matarajio yetu kulingana na kile ambacho utamaduni wetu unafahamu kama njia nzuri na ya kirafiki ya kujitaadhabu. Tunaponelea kuwa mtu ana tabia mbovu isiyotamanika, inakuwa rahisi kudhani kuwa mtu huyo alikusudia kujitaadhabu vivyo hivyo kutoka mwanzoni. Lakini kuna uwezekano kuwa njia yake ya kujitaadhabu inaonyesha tofauti za matarajio ya kitamaduni. Kwa kawaida, ile hali ya kujihisi mgeni na kusitasita huwa katika pande zote mbili: kama ninahisi kuwa mtu au eneo fulani ni tofauti na geni, basi itakuwa sawa kudhani kuwa *mimi* pia naweza kuonekana kama mwenye tabia geni na tofauti.

Ni nani anayechagua kanuni za kuonyesha nidhamu? Mtu au utamaduni unapoonekana kuwa wenye nidhamu au wenye kukosa nidhamu, ni jambo la busara kuuliza swali: kulingana na nini au nani? Mfano mzuri ni Muamerikani aliyedhani kuwa Wakuba ni wakosa nidhamu. Ndio, tunaweza kudai hivyo ikiwa tutaongeza yafuatayo: ikiwa tutatumia ufafanuzi wa Muamerikani, kuwa ni adhabu njema kusema *niwie radhi* au *pole* kila mara mtu anapita kando yako au anapokugonga kwenye foleni, basi Wakuba wote ni wakosa nidhamu. Lakini kama wageni katika nchi ya Kuba, tunapata kuona nidhamu na urafiki kwa njia zingine, katika njia za kikuba. Tunapata hisio kuwa watu ni wenye urafiki, wenye jitihada, wasaidifu, wenye nia ya kukutana na wageni na wenye tabasamu za kupendeza. Zaidi, haiwezekani kuwazungumzia Wakuba au watu wa mataifa mengine kwa ujumla.

Kwa nini tunataka kuwa na nidhamu?

Tunaweza kuwa na sababu tofauti, tunazofahamu na tusizofahamu, ya kutaka kuwa na nidhamu. Kwa mfano, tunaweza kuwa na sababu nzuri ya kutaka mtu fulani awe na fikira nzuri juu yetu, tunaweza taka kuonekana kama wenye kujali, kuonyesha kuwa tumepata malezi mema na labda hatutaki kujiaibisha sisi binafsi na labda wazazi wetu. Lengo moja la kuonyesha nidhamu laweza kuwa kuhakikisha kuwa uhusiano na watu wengine zinadumu, na kuwa yule tunayewasiliana naye anajihisi mtulivu, kuwa anaheshimiwa na kuonyeshwa shukurani, na labda kuwa mtu huyu atafurahia malengo yetu maishani. Kwa sababu tukijifunza kile kinachotakikana na kile kinachovutia, itakuwa kidato cha kwanza katika kujenga kuaminiana, na kuelewana kunarahisisha mno mawasiliano na maelewano. Ni

kawaida katika maisha kuwa kutahitajika kuwasiliana, kufanya kazi, kuelewa, na kueleweka katika njia tunayokusudia.

Lakini kuonyesha nidhamu sio kuonyesha mapenzi au urafiki peke yake; nidhamu yaweza kuwa njia ya kutengeneza umbali kati ya watu. Kuonyesha nidhamu kupindukia yaweza kusababisha kushushwa hadhi, kinaya na dharau.

Je, Wanorwe wanaweza kukosa kanuni za kirasmi, ilihali wawe na nidhamu kwa wakati mmoja?

Mwandishi wa kitabu hiki sio mtaalamu katika masomo ya utamaduni, lakini ni mtu mwenye kiu ya kutaka kujua zaidi, aliyeyapata maarifa masomoni, kazini na kutoka kwa safari katika nchi zingine. Mifano yangu ambayo ni muhimu zaidi ni vikundi vya wanafunzi wa kigeni ambao nimefunza katika Chuo Kikuu Cha Volda katika miaka 17 iliyopita, jumla ya takriban wanafunzi 430 kutoka nchi 77 tofauti. Maandishi kutoka kwa wakaaji wa kigeni na watoto wao yamekuwa pia changa moto kwangu na yameniwezesha kuendelea na kazi hii. Ile hali ya kupatana na watu kutoka tamaduni mbalimbali imeniwezesha kulinganisha na kuweza kuona kwa makini zaidi kuliko hapo awali. Lakini kama Mnorwe na sehemu ya utamaduni wa kinorwe, sio rahisi kuitathmini sehemu za utamaduni wa kinorwe bila mapendeleo. Kwa hivyo nitakapozungumza kuhusu njia fulani za kinorwe za kujitaadhabu, msomaji anaweza kuhisi kuwa maoni yangu yanatolewa kama ufafanuzi na njia ya kujitetea.

Watafiti wanadai kuwa watu kutoka nchi zilizo Ulaya Kaskazini wana fikira nzuri sana ya usawa au ujamaa. Utawala mrefu wa ujamaa na demokratia umeacha alama zake katika nchi ya Norwe (hata kama kufikiri kama mtu binafsi, inayoonelewa kuwa kitu spesheli, hupatikana sambamba na ujamaa). Ndio maana inaonelewa kuwa jambo lisisilopendeza au jambo la kijinga mtu anapojaribu kujigamba kwa kuonyesha wanzake mali yake au cheo chake. Huenda ni jambo hili linalofanya kule kumwuliza Mnorwe kuhusu mapato yake lichukuliwe kama utovu wa nidhamu.

Kama ilivyo desturi, Wanorwe matajiri na waliojulikana sana hupendwa na watu wanapoonyesha kuwa hao ni watu wa kawaida, na kwa kawaida wanaishi kwa njia ambayo ni kinyume na maisha ya utajiri (wanavalia nguo zilizochakaa, wanaendesha motokaa kuukuu) – kwa maneno mengine, wanaonyesha kipimo katika sehemu fulani za maisha yao ili wathibitishie kuwa wao ni watu wa kawaida. Hata Wanorwe matajiri huwa nadra na wafanyikazi nyumbani, na mmojawapo wa wanaume tajiri sana nchini Norwe anaweza kuvua samaki na kuziua bandarini mwenyewe. Vijana katika familia tajiri hawapatiwi kila kitu wanachotaka, na inawabidi wafanye kazi katika wikendi na likizoni ili waweze kujinunulia vitu vya ziada. Aina moja ya tajiri katika nchi ya Norwe anaweza kuwa na jumba la kukodisha katika eneo la milimani linalo bafu 15, ilihali aina nyingine anaweza kuishi katika kibanda kibovu milimani iliyo na choo cha nje, avalie jaketi kuukuu na atumie vifaa vizee katika spoti za kuteleza kwenye theluji. Kwa kawaida, Wanorwe huzipaka nyumba zao rangi, hushona, huchuma matunda na kujitengenezea jemu ya kupaka kwenye mkate, hutayarisha vyakula vyao na kuvipalilia vijishamba vyao, hata kama wao hupata mishahara mikubwa. Ndio maana hatufurahii wageni kutoka nchi zingine wanaotangaza bila ya haya kuwa

hawajawahi kuchafua mikono yao, ama kuwa wana wafanyikazi ambao hutayarisha vyakula vyao.

Upole ni sehemu yetu na kitu kinachotamaniwa sana kati yetu. Tunajivunia kisa kimoja katika kipindi cha ukosefu wa mafuta katika muda wa mwisho wa miaka ya 1970, ambapo Mfalme Olav alisafiri kwa gari moshi (hata ingawa ni wakati mmoja tu, ambao umekuwa maarufu). Waziri mkuu anaishi katika nyumba ya kukodisha na anaweza kutembea bila walinzi wake, watoto katika familia ya mfalme walisoma katika shule za serikali pamoja na watoto wengine, na makanisa na mijengo ya serikali sio yenye marembo kupindukia. Wageni kutoka ng'ambo, kwa mfano, wamedhani mara nyingi kuwa kasri ya mfalme kule Oslo ni kituo cha gari la moshi. Mdadisi mmoja wa kigeni alidai katika kipindi cha runinga muda mfupi uliopita kuwa "upole" wa kinorwe ndio sababu muhimu zaidi inayofanya nchi hii ndogo ipate heshima nyingi sana ya kimataifa, na ikabidhiwe na kuheshimiwa na hadhi ya mleta-amani katika sehemu zingine za dunia. Lakini tunaweza kuona kuwa katika miaka iliyopita, "upole" wa kinorwe na kule kuungana na vikundi vinyonge kumepoteza umuhimu wake. Na ile hali ya Norwe kujulikana kama nchi inayopenda amani inatafsiriwa leo kama hali ya kutaka kujitoshleza; kuwa Wanorwe wanaamini kuwa wao wanajua kile kinachofaa, na kuwa njia ya kinorwe inafaa kuchukuliwa kama mfano bora na dunia yote.

Wazo la umoja na usawa linamaanisha kuwa sio jambo zuri kujigamba mbele ya watu wengine kuhusu watoto wako (ingawa ni kawaida kuwasifu watoto wetu). Maisha ya shule pia yanaonyesha wazo hili. Hadi sasa, masomo hayajatilia mkazo mashindano kati ya wanafunzi: katika shule ya msingi katika nchi ya Norwe, wanafunzi hawapati alama katika mitihani (miaka 7 ya kwanza), mwalimu hataji majina ya wale waliofanya bora zaidi katika mtihani, na matokeo ya mtihani yanapotolewa katika mafunzo ya elimu ya kiwango cha juu, majina hayaonyeshwi waziwazi kwenye orodha.

Kama ilivyo desturi, ile hali ya kuwa Mnorwe haihusu nafasi ya mtu kwenye jamii, lakini inahusu jiografia, yaani mahali ambapo tulilelewa. Mtu ambaye ameishi Bergen kwa miaka 40 atasema kuwa yeye anatoka Voss kama alilelewa huko. Wanorwe wanapokutana na wageni, swali lao la kwanza kwa kawaida huwa: "Unatoka wapi?" Ni baadaye tu ndipo tunaweza kuuliza kuhusu ajira na mahali ambapo mtu hufanya kazi, kwa sababu hatuna haja ya vyeo vya watu, au kuweka watu kwenye viwango tofauti tofauti. Uwezo wa kimaarifa unathaminiwa zaidi ya utajiri.

Wageni hugundua haraka kuwa Wanorwe huwa na njia isiyo ya kirasmi tunapozungumzia lugha yao na njia zao za kujitaadhabu. Wao hukosa urasmi kwa kiwango kikubwa mno kinachoweza kuwafanya watu wengine kuwachukulia kama wakosa nidhamu. Kwa sababu sisi wenyewe hutumia vyeo kwa nadra, sisi husahau umuhimu wa vyeo hivi tunapozungumza na watu kutoka tamaduni zingine. Niliwahi kumkaribisha (katika lugha ya kiingereza) balonzi kutoka nchi ya kigeni kwa Wanorwe wengine. Ingawa tulikuwa kwenye mkusanyiko wa kawaida, alikasirika kwa sababu nilisema *Bwana* na sikutumia cheo chake kabla ya kutaja jina lake. Kwa yeye binafsi, cheo chake na ile hali ya kuifanyia shirika fulani kazi ilikuwa sehemu muhimu ya utu wake.

Kuvaa nguo nzuri ni njia ya kuonyesha nidhamu na heshima kwa wale tulio pamoja nao. Wanafunzi kutoka nchi za kigeni kwa kawaida huvalia nguo za kupendeza mno kwenye karamu yao ya kwanza katika nchi ya Norwe, huvalia suti na tai, au rinda ya kupendeza na viatu virefu. Lakini baadaye, hao huvalia nguo za kawaida, kama wanafunzi Wanorwe, hata ingawa wao huonyesha mshangao wao kwa Wanorwe "matajiri" wanaovalia kwa njia isiyo rasmi. Inawezekana kuwa kanuni za mavazi zinaanza kubadilika nchini Norwe sasa, lakini hadi sasa, imekuwa jambo la aibu kwa mwanamke wa kinorwe kuwa mtu aliyevalia vizuri zaidi kuliko wengine wote kwenye karamu. Mwanafunzi mmoja kutoka Romania alitoa maoni yake, "Hata mabinti-wafalme katika hadithi za kinorwe ni wapole. Hawana rinda za kupendeza wala mapambo, na mfalme ni mkulima bashasha anayesimama mlangoni akiwawazia wanaye."

Kanuni hii isiyo ya kirasmi inaonekana pia katika mahali pa kazi. Wanorwe nchini Norwe hawavalii kwa njia inayovutia wakiwa kazini, hata katika mahali pa kazi ambapo wao hukutana na wateja. Ni vigumu kujua nani ambaye ni bosu na wale ambao ni wafanyikazi wa kawaida kwa kuangalia jinsi walivyovalia. Mwalimu mkuu kwenye chuo cha mafunzo, mkurugenzi wa benki au daktari hospitalini hawahitaji kutokea kwenye mahojiano kwenye televisheni wakivalia suti na tai. Wageni nchini Norwe pia wanaweza kushangazwa, na wakati mwingine kupigwa na butwaa, kwa jinisi Wanorwe wanavyowazungumzia waajiri wao, wakubwa wao, wazazi na waalimu: mpokeaji kwenye kampuni anaweza kumkashifu mkurugenzi mkuu, muuguzi anaweza kumkemea daktari, binti anaweza kumpinga na kumkemea babaye, na mwanafunzi anaweza kutokubaliana vikali na mhadhiri au mwalimu. Katika maoni ya Wanorwe, kama hauwezi kukubali kusahihishwa au kukubali maoni ya watu wengine, basi wewe sio bosu au mwalimu mzuri.

Ni vigumu kupata ishara za vyeo katika njia zetu za maamkuzi na mawasiliano, iwe tunazungumza na mwajiri wetu, mchungaji kanisani, karani au mwalimu (matarajio ya pekee ni kwa familia ya kifalme na raisi wa Bunge La Norwe – Stortinget – wakati yeye yupo kazini katika majengo ya bunge). Njia ya kawaida ya kumwashiria mtu siku hizi ni kusema *du* (njia isiyo ya kirasmi ya kusema *wewe*) kwa kila mtu, na sanasana tunatumia jina la kwanza la mtu au majina yake mawili. Sio jambo la kawaida kutumia vyeo. Kule kutumia maneno ya kuonyesha heshima na njia spesheli za mawasiliano kwa watu walio na mamlaka ni ishara ya kumshusha mtu hadhi, na haiendi sambamba na wazo la usawa. Waajiri wanaowasimamia na kuwalinda wafanyikazi wao, au wanaotoa maagizo mazito katika mahala pa kazi (isipokuwa kwenye jeshi) hawavumiliwi, kwa sababu mtu aliye mamlakani hapaswi kuonyesha uzito wa mamlaka yake kwa wale walio chini yake. Haitoshi kuwa msimamizi kazini ana ujuzi au maarifa ya kufanya kazi yake, msimamizi mzuri lazima awe na uwezo wa kuwasikiliza wengine, awe na huruma, aweze kukubali mawaidha, awe na uwezo wa kujenga timu, aweze kuyatatua migongano na aweze kuwasiliana na kufanya kazi vizuri na wale anaowaongoza. Mfanyikazi wa viwandani kule Ujeremani alitoa maoni yake kuhusu namna ya kufanya kazi ambayo ni kawaida katika nchi ya Norwe na nchi zilizopo Ulaya Kaskazini: "Mwajiri katika nchi zilizopo Ulaya Kaskazini hugawa kazi – na majukumu – kwa wafanyikazi, bila kuwachunguza wakati wote. Wafanyikazi wa kinorwe hupewa jukumu kwa kazi

wanayopaswa kufanya, jambo linalosababisha kuridhika kwa wafanyikazi, na kutengenezeka kwa mahala pazuri pa kufanyia kazi.”

Ingawa sijafanya utafiti wowote unaoweza kuthibitisha madai yangu, ninaweza kusema kuwa tamaduni zilizo na miundo ”iliyonyooka” kama Norwe, zinahitaji kanuni chache zaidi zisizo ngumu kuelewa, kuliko tamaduni zinazotilia mkazo mfumo wa vyeo. Wanorwe hupenda kuamini kuwa wao, hata kama ni juujuu, hawana mfumo wa vyeo ulio waziwazi, lakini huamini kuwa kila mtu ni sawa na anapaswa kuchukuliwa na kuzungumziwa kama mtu sawa. Kwa watu wanaotoka ng’ambo, inaweza kuwa vigumu kuelewa jinsi mfumo huu hufanya kazi.

Tamaduni ”moto” na ”baridi”

Katika utamaduni mgeni, hali ya kutojua kanuni za kijamii inaweza kusababisha kutoelewana, kutoridhika, na inaweza kufanya mtu ahisi kuwa anaonelewa. Kwa kawaida, Wanorwe huamkua kila mtu na *hei, god dag* ama (*go*) *morn* (*Hujambo, u hali gani?* au *siku njema!*). wanafunzi wengine, haswa wale kutoka Marekani Kusini na nchi za kiafrika wametoelewa aina hii ya salamu za juujuu. Baada ya jioni ya kufana na wanafunzi wa kinorwe, wanashushwa wanaposalamiwa siku inayofuata na Wanorwe na *hei* (*hujambo*) ya haraka bila hata ya kusimama. Wengine wanapata ugumu wa kuelewa jambo hili na wanadhani kuwa wanafunzi Wanorwe wanawachukulia hivyo kwa sababu wao ni wageni au kwa sababu wanawadharau. Kwa hivyo inapaswa kufafanuliwa kwa wanafunzi wa kigeni kuwa *hei* (*hujambo*) sio ukosefu wa nidhamu au ukosefu wa urafiki, lakini ni njia ya kawaida ya kinorwe ya kusalamia watu – alama ya kawaida ya nidhamu. Wanafunzi hawa wanatoka kwenye tamaduni ambapo mtu kwa kawaida husimama na kupiga soga kidogo anapokutana na mtu unayefahamu, na hii ni moja wapo ya sababu zinazofanya zijulikane kama tamaduni ”moto”, na si utamaduni ”baridi” kama ule wa kinorwe.

Katika safari ya kikazi katika nchi moja ya kiafrika miaka michache iliyopita, nilipotembelea boma 15-20 pamoja na mwanamume mmoja mwenyeji, nilipata kushuhudia jinsi watu kutoka kwa tamaduni hizi ”moto” huamkuana. Tulipowasili kwenye boma, tulipokelewa mlangoni na memba mmoja wa familia hiyo, na kila wakati kulikuwa na mazungumzo yaliyoendelea zaidi ya dakika chache. Ilikuwa kitu kama hiki: *U hali gani? –Mimi niko salama, ahsante, labda wewe? –Niko salama, ahsante, na mkeo anaendeleaje? –Salama, ahsante, na mkeo je? –Na mamako, na mwanao, na kadhalika.* Kila wakati jibu lilikuwa *salama, ahsante*, hata ingawa mwanamke mkongwe alikuwa anakaribia kuaga dunia katika mojawapo ya nyumba katika boma hilo. Mimi na mazoea yangu ya njia za maamkuzi za kinorwe, niliona haya yote kuwa upuuzi na kazi isiyo na sababu. Majibu yalitoka bila kufikiria na hayakuwa ya kweli, mambo yote yalikuwa kupoteza wakati. Lakini lazima niongezee kitu kimoja ambacho ni muhimu sana; ilikuwa kupoteza wakati kwa *njia yangu ya kufikiria*. Kulingana na matarajio yangu kuhusu jinsi watu huamkuana, na muda na maneno yanayotumika, haya yote yalikuwa bila thamani. Kwangu, njia ya kuamkuana haikuonyesha utamaduni ”moto”, lakini kwa wale watu wawili waliosimama mlangoni, jambo hili lilikuwa la kirafiki, lenye maana, na njia ya heshima ya kuzungumza na mtu – njia ya kuendeleza mazungumzo, labda sawa na jinsi

Wanorwe hujadiliana kuhusu hali ya anga! Swali ni: tunaweza kuzungumza bila mapendeleo kuhusu tamaduni ”moto” na ”baridi”?

Maneno madogo ya heshima – je, ni maneno yasiyo na maana, njia ya kujigamba, au njia ya kuwa na nidhamu?

Tunapotembelea au tunapoishi katika nchi geni, tunaweza kukosa kuyafahamu vyema yale maneno madogo yanayoonyesha kuwa sisi ni wenye nidhamu. Mfaransa anaweza kuhisi kuwa watu wasiosema *bon appetit* kabla ya kula hawajapata malezi bora, na pia kwa mtu anayepita katikati ya watu bila ya kusema *tafadhali nipishe*, hata ingawa ni katikati ya sebule nyumbani, kama tutapindukia kidogo. Na bila shaka kuna sababu kadhaa zinazowafanya wafanyibiashara wa kifaransa kudai kuwa wakurugenzi wakuu kutoka nchi za Skandinavia hufanya kazi nzuri mno, lakini hawana ustaarabu. Wamarekani wametaja kuwa Wanorwe wanaweza kukiacha kikundi cha watu waliokuwa wakizungumza nao bila ya kusema *niwie radhi*, na Waingereza husema mara kwa mara kuwa Wanorwe hujifikiria wao tu. Kwa sababu tunapoulizwa swali *u hali gani?*, tunazungumza juu yetu kwa muda mrefu bila ya kufikiria kuuliza *Na wewe u hali gani?* Na tunaweza kwa urahisi kuongezea mifano mingi zaidi.

”Kumaanisha kwa kweli”?

Wageni wengi wana maoni kuwa Wanorwe ni bahili wa kutumia maneno ya kuonyesha nidhamu. Wanorwe wanaposema na kufanya kitu kinachoonyesha urafiki, hufanya hivyo na nia nzuri na humaanisha kwa kweli. Kama siyoy, hawajisumbui. Chukua barua za kirasmi za kinorwe kama mfano. Wanorwe wanapowasiliana kwa njia hii, kwa kawaida huwa ni na watu wasiowafahamu binafsi. Ilivyo desturi, barua hizi huanza katika lugha ya kiswahili na *Mpenzi Bwana/Bibi*. Lakini barua za kirasmi za kinorwe huondoa maneno kama *mpenzi*, kwa sababu hatuna uhusiano wa karibu na mpokeaji wa barua katika hali kama hii. Na tunapowataja watu siku hizi, tunatumia *Bwana* na *Bibi* kwa nadra sana. Tunapotumia majina haya, huwa ni kama kichekesho: ”Bibi angependa kahawa?” *Bibi* katika lugha ya kinorwe ni neno linalo uhusiano na mwanamke mnene, mwenye umri wa makamu na mwenye kuonyesha uzito wa mamlaka yake. *Bwana* ni jina linalotumika kumtaja Yesu Kristo. Kichekesho kizuri katika nchi ya Norwe ni kutafsiri yafuatayo katika masomo ya lugha ya kifaransa: *Je vais aller à Paris pour chercher le Monsieur qui habite là* hadi yafuatayo: *ninasafiri hadi jiji la Paris kumwona Bwana ambaye anaishi kule*.

Ikilinganishwa na tamaduni zingine, ni bila shaka kuwa, kama inavyodaiwa na wakaaji wengi wa kigeni, kuwa Wanorwe wana maneno machache mno ya kuonyesha urafiki na nidhamu. Lakini ukweli ni kuwa Wanorwe wana maneno fulani yasiyopatikana katika tamaduni zingine, kwa mfano: *takk for maten* (*Ahsante kwa chakula*), inayosemwa mtu anapoondoka mezani. Mwenye nyumba kwa kawaida hujibu: *vel bekomme* (*natumai kuwa ulifurahia*). Mgeni anaporudi nyumbani, ni tabia nzuri kusema *takk for meg, takk for i kveld* (*Ahsante kwa jioni ya kufana*) kwa wenye nyumba, na *takk for laget* (*nimefurahia sana jioni hii pamoja na nyinyi*) kwa wageni wengine ambao amekuwa pamoja nao. Mgeni na mwenye nyumba watakapokutana mara nyingine, au wageni wawili, ni kawaida kusema *takk for sist* (*nilifurahia sana ile jioni ambapo tulikuwa pamoja*). Katika mahali pengine, watu wenye umri wa makamu watasema (*Gud vel-*)*signe maten* ama *signe arbeidet* (*Mungu abariki*

chakula na aibariki kazi yako) wanapokutana na mtu anayekula ua anayefanya kazi. Na kila siku wanafunzi na waalimu huambiana *takk for i dag (Ahsante kwa leo)* kabla ya kuenda makwao. (Kinorwe, kama lugha zingine, inaweza kuonyesha nidhamu kwa njia ya moja kwa moja: *kunne jeg få snakke litt med deg?*) – Tafadhali, ninaweza kuzungumza nawe kidogo?)

Wanorwe wana utamaduni mrefu ya kutumia haya maneno ya kuonyesha nidhamu. Lakini kama wengi walivyosema, tunaogopa kidogo kutumia maneno mapya, haswa kama yanagongana na ile hali ya kumaanisha kile ambacho mtu anasema. Haswa pia kama maneno haya yana mizizi yake katika utamaduni wa kimarekani. Tunayachukulia kama maneno matupu, na maneno ya upuuzi yanayoonyesha udanganyifu na ujinga. *Vizuri kukujua*, ndivyo Wamarekani husema wanapokutana na wewe kwa mara ya kwanza. ”Sawa,” wanorwe hufikiria, ”lakini itakuwaje watasema hivyo, ilihali hawajui chochote kutuhusu?” Ikiwa Wanorwe watasema jambo, lazima kuwe na kusudi, kwa hivyo inaweza kuchukua muda kabla tuzoe maneno mapya ya kuonyesha nidhamu. Lakini tumekuwa na mwanzo mzuri, na ni wale wanaoishi jijini wanaoonyesha wengine wetu njia. Siku hizi ni kawaida kabisa kwa muuzaji dukani kujibu maneno ya mteja *takk for hjelpen (Ahsante kwa usaidizi)* na *bare hyggelig (Ilikuwa raha yangu)* na kumuaga mteja na *ha en fin dag (Kuwa na siku njema)*. Njia hii ya kuonyesha nidhamu inasambaa haraka sana, hata katika maeneo ya mashambani nchini Norwe. *God helg (Kuwa na wikendi njema)* ilikubalika kitambo sana. Lakini wauzaji madukani katika maeneo ya mashambani pia wameanza kusema *ha en fin dag (Kuwa na siku njema)*. Watu wengine hawapendi jambo hili kamwe na husema kuwa ni kujigamba na kuonyesha mapenzi ya kuhadaa, na wakati mwingine huweza kufikiria: ”Hayo hayakuhusu!” au ”Haumaanishi unayoyasema – unasema hivyo tu kwa sababu unazitaka hela zangu.” Pia tunahisi kuwa wauzaji huwa wadanganyifu wanapotumia majina yetu ya kwanza na kuuliza *hvordan har du det? (Waendeleaje?)*, bila ya kuwahi kukutana nasi. Tunadhani mara moja kuwa nia ya muuzaji ya kujaribu kuonyesha ”urafiki” ni kujaribu kutufanya tununue kile ambacho anauza. Mara nyingi, majaribio kama haya huwa na matokeo ambayo ni kinyume na matarajio; urafiki huu wa uwongo unawakasirisha sana Wanorwe, na wengine hata hukata simu.

Hata kama sisi Wanorwe tumeanza ”kugusana” katika miaka kumi iliyopita, bado ni kawaida kuwa hatumkumbatii wala kumbusu mtu ambaye tumekutana naye kwa mara ya kwanza. Tunafanya hivyo tu na watu tunaowapenda kwa kweli na marafiki wa karibu. Na tunapofikiria kumbusu mtu, inatosha kabisa kushikanisha mashavu. Kuamkuana kwa mikono ni kawaida tunapokuana na mtu kwa mara ya kwanza, tunapokaribishwa kama wageni na tunaposema ahsante kwa jioni nzuri pamoja. Katika siku za hivi majuzi nchini Norwe, ni wazi kuwa imekuwa jambo la kawaida miongoni mwa vijana kuamkuana kwa mikono wanapokutana. Jambo hili linaweza kufafanuliwa na kule kukutana na wakaaji wa kigeni na ile hali ya vijana wa kinorwe kutazama filamu nyingi za kigeni.

Tumeshataja kuwa Wanorwe husema *unnskyld (pole/niwie radhi)* kwa nadra. Lakini tunaweza kusema *om forlatelse (niwie radhi)* na *tilgi meg (nisamehe)* ambazo ni aina za kidini za matamshi (tusamehe dhambi zetu). Wakristo Waprotestanti, kama tunavyojua, hawafikii ufalme wa mbinguni kwa sababu ya matendo yao mazuri, lakini kwa sababu ya rehema na

msamaha. Sio vigumu kufikiria kuwa kulipiza kisasi kulikuwa vigumu zaidi kwa wanajeshi wa kale kutoka Ulaya Kaskazini kuliko kumsamehe mtu, tunapojua kuwa ukristo uliletwa miaka 1000 iliyopita. Mtazamo wa binadamu katika dini hii inahusu kukubali kuwa ni kawaida kwa binadamu kufanya makosa, na kwa hivyo anahitaji msamaha. Mwandishi mwislamu aliwahi kutaja mara moja kuwa wakristo wana bahati kuwa na sehemu hii katika dini yao; kulingana na yeye, kule kuonyesha rehema na kuwasamehe watu wanaokiri makosa yao kumekubalika zaidi katika tamaduni za kikristo.

Kuomba msamaha au kuomba radhi hadharani kumefanywa kwa kiwango cha kupindukia nchini Norwe siku hizi: kanisa, waziri mkuu, wabunge, wanasiasa, viongozi na maafisa wengine wa serikali wana tabia ya kuomba msamaha na uelewano kutoka kwa watu – kwa ajili yao na kwa ajili ya makosa yaliyofanywa katika jamii ya kinorwe muda fulani uliopita. Kukiri makosa yao inaamanisha kuwa hawapotezi sura zao, kama Waasia wanavyosema. Wakurugenzi wa makampuni na mawaziri wa serikali huomba, na hupatiwa, rehema na msamaha mara kwa mara, na waandishi wa magazeti na wanahabari wanaweza kuongezea kwa orodha ya makosa ambayo hufanywa. Ni kana kwamba Wanorwe huwahurumia zaidi wale walio mamlakani wanapoonyesha uhafifu wao, kwa sababu hatuna matarajio ya kwamba viongozi na wabunge watakuwa na maadili na uadilifu kuliko watu wengine katika jamii. ”wao ni binadamu tu,” sisi husema.

Ni rahisi mno kugundua mizigo yako ya kitamaduni unapokutana na wageni

Wanorwe hutarajia kuwa sekta ya umma itakuwa tayari kuwasaidia katika njia mbalimbali wanapohitaji msaada. Watu wengine wanaweza kusema kuwa Wanorwe ni wenye bahati sana – na kuwa twatarajia mengi, kwa sababu sisi huwa na fahamu nzuri sana ya haki zetu, na twahisi wakati wote kuwa wenye mamlaka – nchini na katika maeneo madogo – ”wanapaswa kutenda jukumu lao”.

Kwa sababu ya kazi yangu ya ualimu katika chuo kikuu kimoja kilichopo katika jiji moja kule Ulaya Mashariki, ilinibidi niandamane na wanafunzi kwa chakula cha jioni. Kulikuwa na giza nje, kwa sababu nguvu za umeme zilikuwa ghali, kwa hivyo hakukuwa na mataa nje wala katika madirisha ya maduka. Mara ghafla bin vuu, mwanafunzi mmoja akaanguka katika shimo lililokuwa barabarani. Shimo lenyewe lilikuwa na urefu wa karibu futi mbili na halikuwa limezingirwa na ukigo wa aina yoyote. Nilikasirishwa sana, hata ingawa yule msichana aliweza kuendelea na safari akiwa amekasirika kwa njia yake. Katika akili yangu ya kinorwe, nilijiuliza swali: ni nani aliye na jukumu hapa? Nilipokuwa nikifikiri kuhusu maafisa wa trafiki, utawala wa eneo hilo, serikali, kampuni za bima na malipo, yule mwanafunzi wa kibulgaria akanijibu: ”ni sisi tunao jukumu – ni sisi tunaotembea barabarani.”

Kukosa kujua lugha labda ni sababu kubwa ya kutoelewana. Lakini wakaaji wa kigeni wanapoelewa maneno ya kinorwe vizuri sana – vizuri hata kuwaliko Wanorwe wenyewe – mambo yanaweza kuenda mrama. Lugha ya kinorwe ina maneno mengi ya kukopwa kutoka kwa maneno ya kijeremani yaliyotafsiriwa moja kwa moja kutoka kijeremani; ndio maana Wajeremani hujifunza kinorwe kwa haraka, na pia kwa sababu kinorwe na kijeremani zipo katika familia moja ya lugha. Lakini yawezekana kuwa maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya

kijeremeni yatakuwa na maana tofauti katika lugha ya kinorwe. Neno kama hili ni *middag* (*chakula cha mchana*) ambalo linamaanisha *midt på dagen* (*saa sita za mchana*). Neno hili pia linatumika kutaja chakula ambacho kililiwa saa sita za mchana na jamii za wakulima. Siku hizi wasichana na wanawake wa kinorwe husoma na kufanya kazi nje ya nyumba, kwa hivyo hakuna wanaotarajia mabawana wao kurudi nyumbani kwa chakula moto katikati ya siku. Kama ilivyo desturi, mahala pengi pa kazi leo yana dakika thelathini za mapumziko ya chakula cha mchana, na chakula hicho huliwa kazini. Kwa hivyo ni kawaida zaidi kwa familia za kinorwe kula chakula chao cha jioni baada ya kazi, kutokea saa kumi na saa kumi na mbili za jioni, na sio saa sita za jioni, lakini bado twakiita chakula hiki *middag*.

Familia ya kijeremani ambayo ilizungumza lugha ya kinorwe vizuri ilialika wachumba wawili wa kinorwe kwa *middagsmat* (*Mittagessen* – chakula kinacholiwa kati ya saa sita za mchana na saa nane za mchana nchini Ujeremani). Chakula kilitayarishwa kati ya saa sita na saa saba, lakini wageni wao wa kinorwe waliwasili saa kumi za jioni, huku wakiwa na furaha wakisema: ”Tulimaliza kazi mapema mno, hata tukawa na wakati wa kuosha gari tukiwa njiani.” Ingawa hawakusema neno, wale Wajeremani waliwatazamia wale Wanorwe kama wakosa adhabu, na Wanorwe hawakujiwia radhi kwa kufika saa kumi za jioni.

Wanorwe wengi hujisifia ile hali ya ”kusema mambo jinsi yalivyo”, na sio kupiga vijembe, kusema kile unachomaanisha bila ya kusita. Kwa Wanorwe wengi, sio kukosa nidhamu unapoulizia *toalett* au *doen* (*choo*). Twadhani, kwa mfano, kuwa Wamarekani hugeza maana wanaposisitizia kusema *bafuni* au *kwenye chumba cha mapumziko*, ilihali wanachomaanisha ni *choo*. Mnorwe mmoja ambaye hakuwa anafahamu jambo hili aliwasili katika jiji la New York, na akuchukuliwa na gari kwenye kituo cha ndege na marafiki wake. Walimuuliza: ”Wahitaji kuenda kwenye chumba cha mapumziko?” naye akajibu: ”Hapana ahsante, naweza kufanya hivyo papa hapa kwenye gari”.

Ni njia ipi bora ya kusema hapana?

Haitakuwa kweli kudai kuwa Wanorwe wana njia moja tu ya kusema hapana, na hiyo ni kwa kutumia neno *nei* (*hapana*). Kwa kawaida tunapotaka kuonyesha nidhamu, sisi husema *nei, dessverre* (*hapana, naona haitawezekana*), lakini tuna shida ya kuelewa njia bora ya kusema *hapana* bila ya kutumia neno *hapana*. Wanorwe wanaofanya kazi ng’ambo hurudi nyumbani na kusema kuwa watu huko hawawezi kuaminika, wao huahidi kutenda jambo lakini hawatimizi yale waliyoyasema. Lugha ya kimwili, na matamshi yanayoonyesha nidhamu na labda heshima na wema kwa wageni kutoka nchi zingine, yanaweza kufanya majibu yaonekane kama yasiyoeleweka na ya kiajabu – kwa Wanorwe – hata ingawa majibu haya ni sahihi, yenye nidhamu na yanayoeleweka haraka na ”wenyeji”.

Ninakumbuka vizuri sana mfano mmoja wa kutoelewana. Katika nchi ya Senegali kule Afrika Magharibi, nilijihusisha na mradi mmoja wa Shirika la Msalaba Mwekundu ambao ulihusu, miongoni mwa mambo mengine, kununua eneo la shamba. Mwanamume Msenegali aliandamana nami nchini humo. Ni hadithi ndefu, lakini tulipatiwa jina la familia iliyomiliki shamba nje ya mji mkuu Dakar. Tulikutana na mwanamume kutoka familia ile nje kwenye shamba na tukamwonyesha michoro ya mjengo, huku tukifafanua kile tulichotaka. Alikupia kichwa chake kwa yote tulioyasema. Mwishowe, alitabasamu na kusema kwa kifaransa kuwa

ingekuwa hadhi kuu kwake kuuza shamba kwa shirika hili ambalo lilikuwa linafanya kazi nyingi nchini Senegali na katika nchi zingine duniani, na kuwa alitumai kuwa mjengo ungejengwa kama tulivyopanga. Tuliambukana kwa mikono na tukaenda zetu, kwa sababu nilipaswa kuondoka nchini humo baada ya siku chache. Lakini yule mwanamume Msenegali tuliyekuwa naye alinieleza kuwa hatukuwa tumepata shamba lile, jambo ambalo sikuelewa kamwe. Katika hali yangu ya wasiwasi, nilitaka kujitaadhabu kama mwanamke kutoka Ulaya na kurudi na kuuliza: "Jibu ni nini – ndio au hapana?", hata ingawa mwenzangu Msenegali alisisitiza kuwa jibu lilikuwa hapana. Hatukuwa na budi ila kuendelea kutafuta.

Nilichanganyikiwa sana. Niliyaelewa maneno yote ya mazungumzo hayo mafupi, lakini lugha ni zaidi ya maneno. Sikuweza kuzitafsiri ishara za mwili – hali ya sauti yake, kusitasita, kuzungumza kwa macho, mikono, viashirio, kurudiarudia, na upole wake ulivyoonyeshwa katika mawasiliano kati yake na sisi wawili kama wanunuzi katika kisa hicho. Kwa maneno mengine, singeweza "kumsoma" yule mwanamume mpole kutoka utamaduni mgeni, hata ingawa nilielewa maneno aliyoyatamka. Kutafsiri *hapana* ya nidhamu, na ishara zake ambazo mara nyingi hudokezwa bila ya kuonyeshwa waziwazi, huenda ndio kitendo kigumu zaidi cha kilugha ambacho mgeni anaweza kukumbwa nacho. Na alivyonitafsiri, ni yeye pekee yake anayefahamu. Kwa kweli yawezekana kuwa katika hali ya kukutana na watu wengine, ni vigumu sana kutowasiliana, kwa sababu iwe nitatenda jambo au nisitende, iwe nitasema jambo au nikae kimya, hilo linaweza kumweleza mtu jambo fulani kunihusu.

Wageni wanapokosa kusema *hapana* iliyo waziwazi katika majibu yao kwa maswali yetu, kwa kusudi la kuonyesha nidhamu, inaweza kuwa njia ya kuonyesha nidhamu ambayo Wanorwe hawathamini. Tunapomwuliza Mvietnamu au Mmisri njia ya kuenda mahali fulani, na mtu yule hajui njia, atajaribu kutusaidi kwa njia bora awezavyo. Kwa utamaduni wao, ni vibaya kutojaribu, haswaa kama inahusu wageni, kwa sababu ni wageni katika nchi yao na wanapaswa kuonyeshwa wema. Aina hii ya upole yaweza kukuwacha umesimama katika eneo la mji usiofaa. Miongoni mwa mambo ya kwanza ambayo wageni wanapaswa kujifunza nchini Norwe, kwa hivyo, ni kusema waziwazi *ja (gjerne)*(*Ndio (Ningependa hivyo)*) au *nei (dessaerre)* (*Hapana (Naona kuwa haitawezekana)*) wanapojibu maswali na wanapojibu mialiko. Kama sivyo, huenda wakapata maadui au kupata sifa ya kuwa wasioaminika.

Njia ya kinorwe ya kuwa na nidhamu yaweza kupokelewa na watu wengine kama ukosefu wa nidhamu

Kutarajia, kwa Wanorwe, majibu ya moja kwa moja, yaweza kusababisha matokeo kadha wa kadha. Inaweza, kwa mfano, kusababisha watu kutoka Sunnmøre (kaskazini magharibi kwenye eneo la bahari) kuwauwa Waasia – kwa chakula na ukarimu. Mamangu, ambaye hakuwahi kumfukuza yeyote aliyekuwa anauza tikiti za bahati na sibu bila ya kumlisha, alitembelewa siku moja na mwanamume kutoka Korea. Kama ilivyo desturi alikaribishwa kwa chakula moto, na chakula chenyewe kilikuwa kingi, kwa sababu alitaka mgeni ajihisi nyumbani. alipitisha chakula tena na tena, na mwanamume alijiongezea kila wakati. Kama umewahi kukutana na wanawake wenye umri wa makamu kutoka Sunnmøre ambao hulazimisha chakula chini ya koo za wageni wao na kuwakaribisha kwa chakula zaidi, utaweza kutafakari juu ya kisa hiki. Baada ya raundi ya kwanza ya chakula, na raundi zingine

mbili – tatu, Mnorwe anaweza kusema *nei, takk (hapana, ahsante)* ya heshima, na mwishowe itaheshimiwa. Katika eneo nyingi za Asia, kwa mkono mwingine, ni tabia njema kujiongezea chakula kama mwenye nyumba amekukaribisha kwa zaidi, lakini mwenye nyumba kwa kawaida atamtazama mgeni kwa makini na kusimamisha mialiko ya chakula kwa wakati mzuri. Mama alifurahi kuwa mgeni alikipenda chakula, lakini mwishowe alifikiri, ”Maskini, kwa kweli alikuwa na njaa sana.” Bila shaka mgeni alikuwa akifikiri: ”Jamani anapaswa asimame sasa, anapaswa kuelewa kuwa nimekula cha kutosha.” Mamangu pia alimtazama mgeni kwa makini, kwa sababu alimwuliza kama angependa kulala kidogo baada ya chakula, mwaliko ambao bila shaka alifurahia kukubali.

Kubisha mlango ofisini kabla ya kuingia ni alama ya tabia njema nchini Norwe. Katika miaka 17 ambayo nimekuwa nikifunza wageni kutoka nchi za ng’ambo, nimeshuhudia visa kadhaa ambapo wengine wao waliingia ofisini bila ya kubisha. Kukosa adhabu, kukosa heshima, ndio jambo la kwanza ambalo sisi hufikiria – kama hatuwezi kupata ufafanuzi mwingine. Katika nchi zingine za Afrika, ni wezi tu ambao hubisha mlangoni, ili wapate kujua kama kuna mtu nyumbani. Kwa hivyo Biblia ilivyotafsiriwa katika baadhi ya lugha za kiasia, Yesu hangefanywa aseme: ”Tazama, nimesimama mlangoni *nikibisha,*” lakini ”Tazama, nimesimama mlangoni *nikiita.*”

Kusafisha mahali baada ya kufanya kazi inachukuliwa kama tabia njema na kitu ambacho tunajaribu kuwafunza watoto wetu. Kwa kawaida, hakuna mtu nchini Norwe aliye na jukumu la kufagia na kusafisha barabara na mabustani usiku, kama ilivyo katika nchi zingine. Wala hatujazoea kuwa na wafanyikazi nyumbani. Na katika maduka yaliyomo shuleni na kazini, tunapaswa kusafisha meza baada ya kula. Lakini wakati mwingine, tabia yetu nzuri yaweza kutusababishia shida: katika kantini ya chuo kikuu kimoja nchini Bulgaria, mwanamke mmoja mwenye umri wa makamu alikuwa amejikaza kubeba sinia kubwa zilizojaa vikombe na bilauri. Alikuwa anaonekana mchovu, kwa hivyo kwa njia yangu ya kawaida ya kinorwe, nilikusanya vikombe na sahani ambavyo nilikuwa nimetumia, lakini nikakemewa na wanafunzi: ”Kama kila mtu angefanya hivyo, angepoteza kazi yake.”

Viwango vya mishahara ya Wanorwe, na wazo la usawa, yaweza kufafanua kwa nini Wanorwe wanaotembelea nchi zingine wanaweza kuonekana kama wakosa heshima bila ya kujua. Hatufikirii kamwe kuwa mishahara ya wabeba mizigo na wasafishaji katika mahoteli yanaweza kuwa ya chini sana, na hukadiriwa kwa dhana kuwa wao hupokea bakshishi kutoka kwa wageni. Wanorwe wanaweza kuchukuliwa kama baili na wakosa nidhamu wanapokosa kutoa bakshishi kwa huduma za aina tofauti tofauti, kwa sababu hatujazoea kufanya hivyo nyumbani Norwe.

Kuna kanuni za kitamaduni zinazotumika katika utoaji na upokeaji wa zawadi na msaada. Wanorwe wengi huchukia kudaiwa kwa shukrani waliyoonyeshwa hapo awali, kwa hivyo tunavyopokea zawadi au msaada, tunahakikisha kuwa tumelipisha mara tu tunapopata fursa. Wengi wetu hatupendi kuomba pesa, lakini tunapofanya hivyo, tunahakikisha kuwa tumerudisha pesa hizo, hata kama ni kiwango kidogo cha krona 20 na hata kama tumewaomba watu ambao ni matajiri.

Wanorwe wanapopatiana zawadi, haijalishi kama zawadi ni kubwa au ghali, cha muhimu ni kuwa zawadi inafaana na matumaini na matarajio ya anayepokea. Mwanafunzi Mchina aliwahi kusema: "Wanorwe wanapopanga kupatiana zawadi, wao hutumia muda mwingi kutafuta kitu kinachofaa zaidi kwa mtu wanaomfikiria, wakizingatia rangi, kile kilichotumiwa kutengeneza zawadi hiyo na mtindo. Nitakaporudi China, nitachukua nami wanasesere 20 waliovalia nguo za kitamaduni za kinorwe. Nitampa kila mtu barabarani zawadi sawa, kwa sababu ni fikira tu iliyo muhimu." Katika nchi ya Norwe, itakuwa ni kama kukosa nidhamu kutofungua zawadi kama wageni wako pale pale, kwa sababu yaweza kutafsiriwa kama utovu wa shukrani; kuwa hauna shukrani kwa kile ulichokipokea. Lakini Mwasia mwenye nidhamu hawezi kufungua zawadi kama aliyempa zawadi hiyo yupo pale, kwa sababu mgeni ni mwenye umuhimu zaidi kuliko zawadi. Wanorwe wanaweza kumfanya mpatiaji aone haya ikiwa watafungua zawadi kila mtu akiwa anatazama, kama inavyodaiwa na wanafunzi Wachina. Kama zawadi ilikuwa ndogo au isiyo ya thamani, mtoaji Mchina angeona haya. Walitupatia sababu ya madai yao kwa kufafanua kuwa ni jambo la aibu kuwa maskini nchini China, na nyumbani kwao, zawadi isiyo ya thamani yaweza kuashiria umaskini. Wakaaji wengine wa kigeni huwachukulia Wanorwe kama wakosa nidhamu, pale ambapo hawapokei zawadi kwa mikono miwili, na mwanafunzi kutoka Tunisia aliwahi kukiri kuwa Wanorwe wana tabia ya kufanya mambo kupindukia wanapopatiwa kitu fulani: "Wao husema ahsante tena na tena, na huendelea kuusifu uzuri wa zawadi – ni kana kwamba wanastaajabu kuwa mimi ningeweza kuwapatia zawadi kama hiyo!"

Ni utovu wa nidhamu kukataa zawadi, lakini mtu hulazimika kufanya hivyo mara nyingine nchine Norwe. Kazini katika sekta ya umma haukubaliwi kupatiana zawadi juu ya thamani fulani, kwa sababu zawadi zinaweza kuathiri maamuzi yanayohusu mpatianaji na familia yake. Wateja kwa kawaida hawawapatii wafanyikazi zawadi, kwa sababu kila mtu hulipwa mshahara, na inaaminika kuwa mtu atafanya kazi nzuri na kutoa huduma nzuri. Zaidi ya hayo, zawadi zinaweza kutafsiriwa kama rushwa (ufisadi) – kuwa mpatianaji anataka kufanyiwa jambo na mpokeaji.

Wanorwe hushangazwa, kwa mfano, Wairani wanapopigani wenyewe kwa wenyewe kuhusu nani atakayelipia chakula cha kila mtu katika hoteli. Kwa kawaida, sisi hujilipia chakula chetu, wanaume kwa wanawake, isipokuwa wageni ambao ni memba wa familia wa karibu. Wanorwe wanapoletewa bili ya jumla, wao huchukua kalamu na karatasi na kuhesabu kiasi ambacho kila mtu atalipa. Lakini jambo hili halionelewi kama ubaili, lakini kama ishara ya uhuru. Tunataka kulipa katika njia yetu, na hatutaki kumdai mtu chochote. Lakini bila shaka, Wanorwe hupenda kununuliwa kikombe cha kahawa au chakula na marafiki – lakini kwa kipimo, na kwa hivyo ni lazima isemwe waziwazi kuwa ni zawadi. Kama Mnorwe ni mtu mzima aliye na kazi, hatapenda mtu atumie pesa nyingi kwake, isipokuwa mtu huyo ni memba wa familia. Tunahisi kama sisi ni mzigu wa kifedha, na tusio na heshima wala uhuru, tunapomwacha mtu atulipie chakula kwenye hoteli, inayofuatwa na tikiti za mchezo wa kuigiza, maonyesho fulani, tikiti za gari moshi, na kadhalika. Tunaweza kusesitiza kulipisha kitendo hiki kwa wakati unaokuja, kwa sababu tunachukia hisia ya "kununuliwa" au kudaiwa na mtu.

Hapo awali nilitaja kuwa ile hali ya Wanorwe kutojigamba na kutojionyesha inakusudiwa kuwa onyesho la nidhamu. Lakini katika nchi zingine, ile hali ya kujaribu kuonekana mpole au kutojali haileti matokeo jinsi tulivyokusudia. Waziri mmoja wa serikali ya Norwe aliyekuwa akisafiri nchini Japani alikuwa na mtafsiri wake ambaye alikuwa mwanafunzi wa kitambo wa Chuo Kikuu Cha Volda. Katika hotuba yake kwa wabunge wa kijapani, waziri Mnorwe alijitambulisha miongoni mwa maneno mengine na maneno haya: ”Shule ya pekee ambayo nimewahi kuhudhuria ni shule ya mafunzo ya Jumapili kule kanisani.” Mwanafunzi wa kijapani alifahamu maana iliyokusudiwa na yule waziri, na alielewa kuwa waziri – katika njia ya kawaida ya kinorwe – alikusudia kuweka cheo chake chini na kuonyesha kuwa yeye alikuwa mtu wa kawaida. Mwanafunzi alikwepa kutafsiri sentensi hiyo hadi kijapani, akifahamu vyema kuwa tamko kama hilo halingewafanya wenyeji kumwamini na kumheshimu yule mgeni, kinyume na matarajio.

”Ukitaka maisha yako yawe magumu katika nchi ya Norwe, basi chelewa!” ndio habari ambayo mimi hupatia wanafunzi wangu kutoka nchi za ng’ambo. Wanorwe huhisi kuwa ni kuchanganyikiwa na utovu wa nidhamu kuchelewa kufika kwa mikutano ya aina tofauti tofauti na miada, kwa darasa na unapoalikwa kwa chakula cha mchana (ingawa ni sawa kuchelewa kidogo kwa karamu za wanafunzi). Viongozi wa mabiashara, wabunge na haswa familia ya mfalme, huja kwa wakati ufaao kwa mikutano na sherehe. Sisi sote twajua msemu: ”Unapotembelea Roma, fanya vile Waroma hufanya”, lakini kanuni za nidhamu mara nyingi huwa kanuni ambazo hazijaandikwa. Kwa hivyo Wanorwe walioalikwa kwa chakula cha mchana nchini Ufaransa huja kwa wakati ufaao, kama ilivyo desturi nchini Norwe, lakini ni onyesho la nidhamu kwa Wafaransa kwa kisa kama hicho kuja ukiwa umechelewa na karibu dakika 20. Kanuni zetu za kitamaduni za kuonyesha nidhamu zaweza kuwa ngumu kupuuza hata tunapoishi katika jamii ambapo tunafahamu kuna tamaduni tofauti. Dadangu, ambaye ameishi miaka 26 katika nchi iliyo Yuroopa kusini, amekasirishwa kwa miaka mingi na ile hali ya watu kukataa kuheshimu makubaliano na kufika kwa wakati mzuri mtu anapoalikwa. Kwa sababu anapowaalika wageni kwa chakula cha mchana saa mbili za jioni, hawaji hadi masaa mawili baadaye. Yeye na bwana yake kwa kawaida hualikwa kwa chakula cha jioni saa mbili, na dadangu husisitiza kuja kwa wakati unaofaa, hata kama wenyeji huenda wako sokoni au bafuni wanapowasili. Yeye hukasirika kila wakati!

Wanafunzi wa kigeni na wakaaji wa Norwe kutoka nchi zingine wanaisifia sana njia ambayo wanorwe wanajitaadabu

Katika insha na kazi zingine za kuchapishwa zilizoandikwa na wanafunzi wa kigeni na wakaaji wa kigeni, ni jambo la kufurahisha kuona ni sifa zipi, mitazamo ipi na thamani zipi ambazo wanaonelea ni kawaida na Wanorwe. Katika sehemu hii, mifano itakuwa kama chanzo na ufafanuzi wa utovu wa nidhamu, au kuonyeshwa kwa nidhamu kwa Wanorwe, kwa njia iliyo pana zaidi.

Wengi wamegundua kwamba Wanorwe husherehekea siku ya kuzaliwa (sio siku ya majina), na kuwa Krismasi na tarehe 17 Mai (Siku Ya Katiba, ambayo ni sikukuu nchini Norwe) ni siku muhimu, ”kuwa wao hutumia nguvu nyingi za umeme, hulipa kodi na huamini sana kuwa mazungumzo yanaweza kutatua shida za aina zozote.” Wanorwe kwa ujumla

hawajishughulishi na mashindano, lakini wanaogopa kupoteza haki ya kuyaamua maswala yao wenyewe, na wanashuku sana ujumuishaji wa mamlaka. Watu katika nchi hii hulalamika sana, hata ingawa wanaamini kuwa Norwe ndio nchi bora zaidi duniani ya kuishi. Ni kawaida kwa Wanorwe kumiliki nyumba baharini au milimani, kusoma magazeti popote walipo, kutoa viatu wanavyomtembelea mtu, kula viazi, kunywa maziwa na kahawa nyingi mno, kula nafaka za kusagwa kama kiamsha kinywa na uji jumamosi, na kuchunga meno yao vizuri. Wanorwe huketi nje kwenye jua mara wapatapo nafasi na huenda likizoni katika nchi zenye joto. Wanaogopa kunenepa, "kwa hivyo hukimbia pamoja na mbwa wao." kila mtu ana haki ya kuokota zabibu na uyoga, kuogelea na kutembea, hata katika eneo zinazomilikiwa na familia binafsi au wakulima. Kuna sheria kali za kuendesha kama mtu ni mlevi, lakini hakuna sheria zinazomzuia mtu kunywa kiwango kikubwa cha pombe karamuni. Wanorwe kwa kawaida hawazungumzii maswala ya dini, na wachungaji kwa kawaida hawasomi Bibilia kwenye basi ("kwa nini Wanorwe hupewa Jumapili kama siku ya mapumziko, iwapo hawaendi kanisani?"). Watu wa Norwe wanajivunia spoti za msimu wa baridi, mazingira na hewa safi. "Wao ni wapenda amani kwa sababu wao ndio hukabidhi Taji la Amani la Nobel," na wao hutoa pesa nyingi kwa miradi ya kuchanga pesa kwa ajili ya kuwasaidia watu wasiojiweza.

Wanaume na wanawake wa kinorwe kwa kawaida hawagombani hadharani (isipokuwa kama wamelewa) na ni vigumu kwa wao kuzungumza na watu wasiowafahamu. Mwanafunzi Mromani aliwahi kuandika kwenye insha: "Mambo sasa yananiendea vizuri humu nchini Norwe, kwa sababu mimi sasa nimekuwa mtu asiyezungumza na watu wengine. (...) Waasia na Wanorwe wote ni wenye kunyamaza, jambo linalomaanisha kwamba hawatawahi kukutana kamwe!" Wengi wamefahamu kuwa Wanorwe hujitaadhabu kwa njia tofauti kabisa wanapotembea kwenye misitu au maeneo ya mashambani yaliyo nje ya eneo kulipo watu. Wakiwa huko, huwaamkua kila mtu wanaokutana naye, na hata husimama na kupiga soga kidogo na watu wasiowafahamu kamwe.

Uhakika kuwa Wanorwe wana uhusiano mwema na mazingira ni alama ambayo wageni wengi huachwa nayo baada ya muda mfupi tu katika nchi ya Norwe. Mwanafunzi wa kiingereza anafafanua hivi: "Wanorwe Nansen na Amundsen walikuwa wa kwanza kufika kwenye ncha ya kaskazini na ncha ya kusini, sio watu kutoka nchi 'shujaa' Uingereza. Hawa wavumbuzi ni kielelezo na mfano mwema, na wanaume na wanawake Wanorwe wasipokuwa na matembezi marefu katika siku ya Jumapili, huwa na dhamira mbaya. Wao hujifurahia sana wanapokuwa na matembezi hatari milimani, na kama inavyoonekana bora, Wanorwe wanapaswa kulowa maji, na kuhisi baridi na njaa wanaporudi nyumbani." Mwanafunzi kutoka Venezuela anapata vigumu kuelewa kwa nini Wanorwe "hutembea kilomita nyingi milimani ili watafute miamba fulani na nyasi. Wao hutaka sana kuwa peke yao juu ya mlima na hubeba chakula na kinywaji kutoka nyumbani.

Kwa sababu nchi ya Norwe inajivunia eneo kubwa la pwani linalopaka na Bahari ya Kusini, hali ya anga hubadilika haraka. Kipimo cha joto, mvua na upepo ni muhimu sana kwa wakulima na wavuvi, na Wanorwe wanapoandaa jambo lolote litakalofanyika nje, huwa muhimu kujua utabiri wa hali ya anga. Hali ya anga ni jambo salama la kuzungumzia,

lisilokuwa na uhusiano wa kisiasa au migongano, kitu ambacho watu wote hushuhudia. Mwanafunzi kutoka Thailand alitoa maoni yake kuhusu jinsi Wanorwe huanza mazungumzo kwa kutaja hali ya anga – jinsi hali ya anga ilivyo leo ikilinganishwa na jana, au mwaka uliopita kwa wakati kama huo, na jinsi inaweza kuwa jioni au kesho. Aliendelea kusema: ”Riwaya nyingi za kinorwe hutoa maelezo juu ya mazingira na hali ya anga, an utabiri wa hali ya anga katika redio na televisheni ni muhimu sana kwa Wanorwe. Wao huangalia utabiri wa hali ya anga mara kadhaa kwa siku, na wengine huandika yote kuhusu kipimo cha joto na mvua kwenye shajara. Kule Thailand hatuzungumzi kuhusu hali ya anga, kwa sababu huwa sawa wakati wote, lakini nchini Norwe, hata *mimi* nimeanza kuwaza juu ya upepo na kipimo cha joto. Siku moja nilimwuliza mamangu kuhusu hali ya anga kule Thailand. Alishtuka sana na akahofia kuwa kungekuwepo na dhoruba na akauliza: ”Umepashwa habari kuhusu jambo nisilolifahamu?”

Wakaaji wengi wa kigeni hulalamika kuwa hunyesha sana, na wengine hudhani kuwa ”Wanorwe wote huvaa jaketi zenye kofia, na hata watoto wadogo huwa na miavuli.” Mwanafunzi mmoja Mturkia ambaye alionelea ni bora kukaa ndani pale ambapo kipimo cha joto cha hewa kilipokuwa gradi 10 aliandika: ”Watoto wa kinorwe huचेza nje hata kama kuna upepo na mvua. Wanaume na wanawake wa kinorwe pia hukimbia nje hata kama kuna theluji chini. Wao huwa na matembezi katika hali zote za anga. Hata wanawake waja wazito, watu waliopita umri wa miaka 80 na watoto wa miaka 4 wanaweza kuenda kwa matembezi marefu kwa kusudi la kushiriki katika spoti za kuteleza kwenye theluji.

Wakaaji wengine wa kigeni wameleta kutoka nchi zao utamaduni wa kumaliza siku au wiki ya kazi kwa kunywa pombe pamoja na wafanyikaza wengine baada ya kazi. Wanorwe wanaweza kuonekana kama wanyamavu wanapotembea kujiunga nao. Lakini utamaduni huu sio wa kinorwe, kwa sababu baada ya kazi, wanaume na wanawake wote huwachukua wanao kutoka shule au vituo vya kuwachunga watoto baada ya shule, hununua bidhaa kadhaa na hutayarisha chakula cha jioni, kabla ya kuharakisha ili kujiunga na mazoezi ya kwaya, kituo cha mazoezi, mkutano wa kisiasa au jumuiya fulani baadaye jioni.

Wanafunzi wengine hulinganisha Norwe na nchi zao, na huonelea kuwa madereva wa mabasi nchini Norwe ni wachangamfu na wasaidifu zaidi, na kuwa madereva wa kinorwe kwa ujumla ni wenye nidhamu zaidi kwa wapita njia. Wao husimama hata pasipo na mahali pa kuvukia kwa wapita njia. Wengi huonelea kuwa ni jambo zuri sana kuwa madereva nchini Norwe hawapigi honi. Kitu kingine ambacho watu huonelea ni kizuri sana ni kuwa wamiliki wa mbwa huwafunga mbwa wao kwa kamba wanapotembea, na kuwa wengi huchukua vinyesi vya mbwa wao nyumbani nao kwenye mfuko wa plastiki kutoka kwenye barabara, au kwenye bustani.

Mifano iliyotolewa na wanafunzi wa kigeni kuhusu tamaduni za kinorwe za kushangaza ni kuwa Wanorwe huwasha mishumaa kwenye meza wakati wa kula hata kama ni msimu wa jua, hupamba mti wa krismasi kwa bendera ndogo za kinorwe, huzungumza kilahaja hata ingawa wamepata elimu ya juu na huimba nyimbo za kisasa kwa lahaja au kiingereza, hupaka nyumba zao rangi za aina zote zipatikanazo chini ya jua, hupanda nyasi kwenye paa za nyumba na hujenga jukwaa za mbao kwa sanduku zao za barua na pipa zao za takataka.

Kitu kinachoshangaza mno, kwa maoni ya wengi, ni likizo ambayo wanaume hupata, huku bado wakipokea mshahara mzima, pale ambapo mwana huzaliwa katika familia, na kuwa shirika la kushughulikia masilahi ya watoto inaweza kuwanyang'anya wazazi jukumu la kuwalea watoto ikiwa hawatapati malezi bora. Watoto wote kati ya umri wa 0 na 16 wana haki ya kupokea masilahi yote ya watoto hata kama wazazi wana hali mbaya ya uchumi. Ni jambo la kushangaza pia kuwa wazazi na waalimu wanaweza kuadhibiwa ikiwa watawachapa watoto watundu. Wanafunzi wengine huuliza kama ni kweli kuwa mwanamume anaweza kutiwa mbaroni kwa kumchapa bibiye au bintiye, na kama vijana wa kinorwe wanaweza kuwa na wapenzi wengi kabla ya kufunga ndoa. Wanafunzi wa kiume wameshuhudia kualikwa kwenye densi na wasichana wa kinorwe bila ya hiyo kuwa mwaliko kwa kitu zaidi ya hapo, na wengi wameelewa kuwa Wanorwe hawataki kufunga ndoa na kupata familia, kuwa watoto wadogo wanapaswa kulala mapema, ndio maana hawawezi kuonekana nje wakila chakula cha jioni pamoja na wazazi wao kwenye hoteli.

Inaweza pia kuonekana kama jambo la kushangaza kuwa wanaume Wanorwe husalamiana kwa mikono na wanawake na sio na wanaume wengine peke yake, kuwa wanaume Wanorwe huosha sakafu, hupika mkate na wanaweza kufanya kazi kwenye shule ya watoto wadogo. Hakikisho kuwa mashoga wa kiume na kike wanaweza kuwa wachungaji kanisani, na kuwa Norwe ina askofu wa kike, yaweza kuwakasirisha wageni wengine. Inashangaza pia kuwa jela nchini Norwe zinafanana na vyumba vya kupendeza vilizo na tarakilishi na televisheni, kuwa ni lazima waziri mkuu apige foleni kwenye kitua cha posta pamoja na watu wengine, na kuwa mfalme anaweza kutembea huru barabarani au kuendesha gari waziwazi. Wengine hushangazawa na nyumba za Wanorwe, "hufanana na makavazi na mapambo ya aina yote na picha ukutani mwote". Wengine hushangaa kuwa ni lazima ualikwe ili utembelee familia ya kinorwe Jumamosi jioni. Kuwa kupiga kambi, kupika na kushona ni mafunzo shuleni, na kuwa Wanorwe huonelea kuwa husiano za kibinafsi katika maisha ya kikazi kuwa alama ya ufisadi. Wengine huonelea kuwa kaburi na bustani za maua nje ya majumba ya kuwachunga watu wakongwe nchini Norwe "hufanana na bustani za wapenzi wala sio makaburi na nyumbani kwa wagonjwa."

Huleta hisia mbaya kuwa wazazi wakongwe na ahali huishi katika nyumba za kuwachunga watu wakongwe, na kuwa familia hazionyeshi umoja, na kuwa vijana wengi wa kinorwe hawajishughulishi na siasa. Wengi wana maoni makali kuhusu jinsi wafungwa wanavyolindwa, hudhani kuwa polisi ni wa kudanganyika kirahisi, na kuwa watu na wanahabari huangazia ngono kupindukia. Kuongezea, wengi huonelea kuwa Wanorwe huogopa sana kuadilisha, kwa kiasa kinachowatoweza kupeana mawaidha, kuwa wao huaibika wanapoeleza kuwa wanazungumza kiingereza kizuri mno, na kuwa wao huvalia nguo katika njia isiyofaa wanapokuwa kazini. Wengi huonelea kuwa jamii ya kinorwe imejaa sheria na kanuni, kuwa mambo mengi hayaruhusiki na kila kitu kinapaswa kufanywa haraka, ili mtu awe dhabiti na mwenye manufaa. Na cha kuongezea ni kuwa, msimu wa jua wa kinorwe unasifiwa kupindukia!

Mara nyingine twashangazwa na shukrani inayoonyeshwa kwa vitu ambavyo sisi Wanorwe huchukulia kama vya kawaida. Mifano ni: Wanorwe wanaweza kupata riziki yao kwa kuwa na kazi moja tu, wanawake wanaowalea watoto peke yao na watu waliotalikiana huheshimika

katika jamii na pia huchaguliwa kama mawaziri serikalini, Wanorwe wanaweza kuwakashifu wanasiasa, maaskofu na watu wengine mamlakani bila ya kuogopa kuteswa, watu walemavu wanaweza kupokea elimu, kila mtu anayetaka kusoma ana haki ya kupata msaada wa kifedha kutoka kwa serikali, na waalimu hawana tabia ya kutafuta makosa tu, wao huangazia pia sehemu nzuri za kazi ya mwanafunzi. Wengi wamesema jinsi wamependezwa na kushangazwa na jinsi wanasiasa wanaume katika bunge ya Norwe – Stortinget – wanapatia familia zao kipaumbele, huku wakizisahau ndoto zao za kisiasa. Tunapozungumzia maisha ya familia ya kinorwe na jukumu za kijinsia, kwa kawaida huwa hali ya mwanamke inayoangaziwa sana; kuwa ni msichana au mwanamke ambaye huamua kama anataka kutoa mimba au la, kuwa bibi anaweza kutokubaliana na bwanaye mbele ya watu wengine na kuwa ”yeye anaweza kuketi kwenye sofa na kumwacha bwanaye amwandaliye yeye na marafiki wake chakula na vinywaji”. Ni kawaida kwa mwanamke kumtaliki bwanaye kama ilivyo kawaida kwa mwanamume kumtaliki bibiye, na bado huwa na haki sawa na bwanaye kuhusu watoto wao na urithi wa mali. Inajulikana wazi kuwa kaka wa kinorwe hawezi kutoa maamuzi kuhusu dadake na kuwa hana haki ya kumchapa, kuwa wasichana na wavulana wa kinorwe wako huru (katika umri wa 15 wanaweza kuwa memba wa jumuiya na kuamua kuhusu elimu yao na dini), na wasichana na wavulana wanaweza kuwa marafiki wa karibu bila ya mtu kuwasengenya. Huwa jambo la kushangaza kwa wanafunzi wa kigeni kuwa wanawake wanaowalea watoto peke yao na wanawake waja wazito wanasoma katika chuo kikuu, kama ilivyo jambo la kawaida katika nchi hii, na ”ni katika nchi ya Norwe peke yake ambapo mama aliyepata mtoto nje ya ndoa, angefunga ndoa na mwanamfalme na kuwa malkia mtarajiwa wa nchi”.

”Labda wanaume wa kinorwe wana uchekekaji tofauti kuliko wanaume kutoka nchi zingine,” akaandika mwanafunzi mmoja kutoka Lebanon, na akendelea: ”Rafiki yangu mmoja alikuwa kweneye bustani moja mjini Bergen na katika ubao aliokuwa ameketia, kulikuwa na mwanamume mmoja mlevi aliyekuwa anakunywa pombe. Watu wawili, bibi na bwana, wakaja alipokuwa ameketi, na mwanamume mlevi akawapungia na chupa chake cha pombe na akamweleza yule mwanamume: ’Nampenda huyo manzi wako!’ Huyo bwana alitabasamu na akajibu: ’Mimi pia’.”

Mwanafunzi mwingine alipigwa na butwaa kwa yale aliyoyasoma kwenye gazeti (2004): ”Mgeni katika hoteli ya kinorwe alimchapa mhudumu wa kike kofi kwenye mgongo alipokuwa anatembea kando yake. Huyu mwanamume alilazimishwa kumpatia krona 6000 kama malipo!”

Uhusiano kati ya wazazi na watoto pia huleta hisia: Watoto wa kinorwe wanaweza kuzungumza na wazazi wao kuhusu chochote kile, na wazazi huzungumza na wanao kuhusu miili yao, magonjwa, maswala ya ngono na kifo. ”Wazazi wa kinorwe hawaachi kuwapenda wanao kama wao ni mashoga au wanapopata watoto nje ya ndoa, au hata wanapovunja sheria au kutumia madawa ya kulevya:”

Wakaaji nchini Norwe huchukulia kama jambo la kawaida kuwa ”serikali huonyesha upole kwa watu wa nchi hii”, kama mwanafunzi mmoja mwasia alivyosema. Miongoni mwa mambo mengine, alionelea kuwa sio jambo la kawaida kuwa Siku Ya Katiba mnamo 17 Mai inaweza kusherehekewa bila gwaride la wanajeshi, au kuwa watu hujaribu kuwasaidia watumiaji wa madawa ya kulevya, huchukua hatua kuhusu vita vya kinyumbani na huwahukumu wale wanaowanajisi wanawake na watoto, na haya yote hufanyika nchini Norwe. ”Kitu kimoja ambacho ni kizuri sana katika utamaduni wa kinorwe ni kuwa anayenajisi ndiye hubeba aibu na hatia, na sio msichana au familia yake.” Alionelea pia kuwa ni jambo zuri kuwa serikali na makampuni ya kibinafsi huwapa wafanyikazi likizo ya wiki

tano, huku mtu akipokea malipo yote (na wiki sita kwa wale zaidi ya miaka 60). Mwanafunzi kutoka Lebanon alidai kuwa serikali ilitoa huduma nzuri mno pale ambapo helikopta ilikuja kumwokoza rafiki yake baada ya ajali milimani, na pale ambapo hospitali ilifanya upasuaji kwa kifundo cha mguu wake bila ya kuulizia jina lake, nchi aliyotoka au kama alikuwa na mpango wowote wa bima. Wengi wametoa maoni kuhusu maelewano ya kiutu yanayoonyeshwa katika nchi hii pale ambapo wanatoa matibabu kwa magonjwa ya kiakili, na kuwa watu wanaojaribu kuchukua maisha yao hawatiwi mbaroni, lakini hupatiwa uangalizi na msaada wanayohitaji.

Inapohusu maswala ya utovu wa nidhamu miongoni mwa Wanorwe, wanafunzi wa kigeni hufanya kimasomaso mwanzoni. Sio kila mtu anayependa kutoa maoni yake kuhusu utovu wa nidhamu, kwa sababu hiyo ni kukosa nidhamu! Lakini polepole, mambo fulani hutajwa: kutumia vichokonoo hotelini ni jambo la kushangaza na huchukuliwa kama utovu wa nidhamu na wageni wengi. Wanorwe wengi hawasifiani kuhusu jinisi walivyovalia, wanaweza kusimama na mikono mifukoni wanapozungumza na mtu, wahudumu Wanorwe hutupa sahani mezani, ishara katika nchi hii ni jeuri (Hakuna kuingia!), Wanorwe huvalia nguo za spoti wanapokuwa wageni (watalii) katika nchi zingine, na ”ni jambo la kushangaza kuwa unapomba krona 10 au mshumaa kutoka kwa Mnorwe, wao hutaka warudishiwe hata ingawa wao ni matajiri sana na humiliki mishumaa mingi.” Wageni wengi huzungumzia ”tabia za kinorwe mezani” wanapozungumzia jinsi Wanorwe hujitaadhabu mezani. Katika tamaduni zingine mtu humwomba aliyeketi kando yake kumpitishia chumvi, ”lakini Wanorwe hunyoosha mkono juu ya chakula cha aliyeketi kando yake na kuchukua chumvi mwenyewe, bila hata ya kusema ’Niwie radhi’.”

Ile hali ya kuzihukumu tamaduni na mazoea ya kinorwe inategemea macho yanayotazama

Ni kawaida kwa watu wawili wanaotoka katika mji au familia moja kuwa na maoni tofauti kuhusu njia za kujitaadhabu na vipengele vya utamaduni, kwa sababu takaramu na vipaumbele hujenga msingi wa hukumu zetu kwa njia sawa kama vipeo na desturi fulani za utamaduni.

Wanafunzi kutoka nchi moja wanaweza, kwa mfano, kutokubaliana vikali kuhusu swala la kutoa adhabu katika nchi ya Norwe. Wengine hufikiri kuwa ”ni kawaida kabisa kwa nchi inayotoza taji la amani la Nobel kutotumia hukumu ya kifo”. Wengine huamini kuwa hukumu ya kifo yaweza hitajika wakati mwingine na kuwa ”miaka 21 kama hukumu ya jela iliyo juu zaidi ni kipimo kidogo sana, haswa tukizingatia kuwa wengi wa wafungwa nchini Norwe hukamilisha 2/3 tu ya kifungo chao”. Katika nchi ya Norwe watu chini ya umri wa 15 hawawezi kufungwa jela, lakini wanafunzi wengi wanaonelea kuwa kifungo cha jela kinapaswa kutumiwa kama kizuizi kwa watu wa umri zote. Wengine wanaonelea kuwa ”katika nchi huru kama Norwe”, kuua kwa huruma au *euthanasia* yapaswa kuwa halali.

Kile kinachoonelewa kuwa ishara ya imani na mamlaka na kile kinachoonelewa kuwa sifa kubwa hutofautiana kwa kawaida kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Imeshatajwa awali kuwa kukiri makosa yako inakubalika kabisa nchini Norwe; inaweza pia kuwa jambo zuri la kufanya ili kuongeza imani, na jambo hili linagusia wanasiasa na viongozi wa biashara kwa njia sawa na watu wa kawaida. Lakini ”kuweka kadi zako zote mezani” yaweza kutazamiwa kwa njia tofauti kabisa katika tamaduni zingine. Mwanafunzi kutoka Yapani aliandika, ”ni jambo la aibu kwa Wayapani kusikia kuwa walio mamlakani nchini Norwe hukiri makosa yao waziwazi”, na mwanafunzi Msomali alijumlisha kuhusu utamaduni wake

alipoandika: "Hatuwezi kamwe kuyakiri makosa yetu, kwa sababu jambo hili lasababisha aibu kubwa. Ikiwa utakana kutenda makosa, basi waweza kutembea na kichwa chako juu".

Wakaaji wengi wa kigeni wametaja kuwa Wanorwe ni watu wanyamavu sana, hawazungumzi kwa sauti ya juu kwenye benki, madukani au kwenye basi wanapomwona mtu wanaomfahamu, hawaneni zaidi ya inayotakikana kwa abiria wenzao katika basi au gari la moshi, na hawatembeleani kamwe bila mwaliko. Tutatafsiri unyamavu huu kwa njia gani? Kama dharau? Kama kuonyesha hisani? Wakaaji wa kigeni huonelea kuwa njia nzuri ya kuwaamkua watu ni kusimama na kupiga soga kidogo, kuhusu familia au mambo haya au yale. Mwanafunzi mmoja kutoka Urusi ana maoni ambayo ni kinyume: "Inanifaa sana kuwa Wanorwe hutabasamu tu na kusema *hei (hujambo)* tuanpokutana. Hapa ninaweza kujihifadhia maisha yangu ya kibinafsi. Sipendi jinsi watu kule nyumbani huwa na maswali mengi na humhoji mtu. Kile wasichojua, hukisia, na wanaweza kuanzisha minong'ono. Mwanafunzi kutoka Uhabeshi alisema kuwa kule nyumbani, watu wanapaswa kuacha kutumia kanuni ndefu ambazo Wahabeshi hutumia wanapokutana na mtu. Anapoenda nyumbani kwa likizo, hawezi kuenda popote, kwa sababu marafiki na watu wanaomfahamu wanataka kuzungumza – na kunywa kahawa. Mazungumzo yanaweza kuchukua asubuhi nzima, na anahofia kuwa nchi hiyo haitaweza kuendelea hadi wakati ambapo watu wataanza kuwa dhabiti zaidi.

Wakati fulani uliopita, familia moja ya kigeni kutoka Moroko ilihamia eneo la makazi la ujumla kule Kristiansand na walitarajia kuwa majirani wangewatembelea na chakula au zawadi ndogo kama njia ya kuwakaribisha. Haikufanyika, na mke wa familia hiyo alionelea kuwa ilikuwa jambo la kuhuzunisha na utovu wa nidhamu; hakuhiisi kama amekaribishwa. Wakaaji wengine wa kigeni ambao wameshuhudia visa kama hivi wanaweza, lakini, kutazama jambo hili kwa njia tofauti: "Kwa kweli ni vizuri kuwa majirani hawakutembelea na kutuletea chakula na kuzungumza sana, kwa maana sisi tuna kazi nyingi ya kuhamisha vitu vyetu na kuna vijisanduku na mifuko kila mahali".

Waakaji wengine wa kigeni huonelea ni jambo zuri kuwa Wanorwe ni wanyamavu, lakini wengine wanadhani kuwa Wanorwe hawaonyeshi hisia zao. Mwanafunzi mmoja Mwamerikani alikuwa akisafiri kwenye basi kwenye barabara nyembamba yenye kuzingamana, kule magharibi mwa Norwe, huku kukiwa na mteremko kwenye upande wa kulia uliopakana na maji ya bahari. Basi lilisimama pembeni, na Mwamerikani alipigwa na butwaa alipoona gari likining'inia kwenye gurudumu moja ukingoni mwa barabara, huku likikaribia kuteleza majini na kuzama. Alitoka nje mbio ili aone kama kuna jambo ambalo angeweza kufanya ili kusaidia, huku abiria wa kinorwe wakiketi bila ya kuonekana kama wamesumbuliwa na chochote, wakizinyosha shingo zao ili wajue sababu ya basi kusimama, na wakaendelea kuketi huku wakingoja safari iendelee.

Wageni wengine wanaweza kuwa na hisia mbaya wakati ambapo watoto na vijana wa kinorwe wanakosa kusimama na kuwapa watu wakongwe viti vyao kwenye basi. Ni tabia njema kufanya hivyo, lakini huenda kuwa vijana hawa wameshuhudia kuwa watu wakongwe wa kinorwe mara nyingi hukataa mwaliko kama huo. Sababu moja la jambo hili laweza kuwa hawataki kuonekana kama watu wazee na dhaifu, na kwa kweli Wanorwe wakongwe kwa kawaida huwa katika hali nzuri ya kimwili.

Watoto na vijana wa kinorwe hujaribu kwa nadra kuonyesha heshima kwa watu wazima walio pamoja nao. Tunaweza kwa kweli kujadiliana kama huu ni ukosefu wa nidhamu, lakini wengi wa Wanorwe wanaweza kukubaliana kuwa kuna tofauti kati ya heshima na woga. Watoto wengi wanalelewa kutokubaliana na watu wazima iwapo wanashuhudia jambo ambalo wanahisi ni dhalimu au linaloonyesha utovu wa nidhamu. Wengine wanaweza

kukueleza kuwa huku ni kupindukia. Katika tamaduni nyingi, ni jambo dhahiri shahiri kuwa unapaswa kuwasiliana na watu wazima kwa njia ya nidhamu. Wanorwe wengine hukubaliana, lakini sio wote kwa hakika. Wengine hudai kuwa watu wazima wanapaswa kuheshimiwa iwapo wanastahili heshima hiyo, kwa sababu watu wazima wengine ni wenye kukasirika haraka na wenye mtazamo mbaya, wenye kuhakiki na wenye mapendeleo, na wanaolalamika wakati wote kuhusu vijana, - kwa hivyo, kwa nini tuwasiliane nao kwa njia ya heshima? Kwa kuongezea, heshima inahusisha watu katika pande zote, watu wazima wanapaswa kuheshimu na kuonyesha upole kwa watoto na vijana pia.

Wanafunzi wengine wa kigeni huchukulia kama jambo la kawaida kuwa wao hupatiwa mahali pa kuishi katika hosteli nchini Norwe, wakati ambapo wanafunzi wengine kutoka ng'ambo huhisi kuwa ni umaskini na upweke kuishi peke yako kwenye chumba. Wakaaji wengine wa kigeni huhisi kuwa ni kutoajibika kuwa watoto wachanga wa kinorwe hulala chumbani peke yao walipo na umri wa wiki chache tu, na kuwa vijana wa kinorwe huendesha habari za fedha zao katika umri mdogo na hutoa maamuzi kuhusu maisha yao. Wengine huona kuwa ni jambo la kushangaza kuwa Wanorwe hawalipii masomo ya wanao, kuwa wanawawacha wahamie makao yao madogo katika umri wa 18-20, kuwa hawawezi kutoa maamuzi kuhusu jinsi wanavyotumia wakati wao na watu wanaokaa nao kama marafiki. Ufafanuzi mmoja waweza kutolewa na utafiti uliofanywa na jarida la kinorwe "Samfunnsspeilet" mwaka wa 1998 ambao ulionyesha kile ambacho wazazi 1127 wa kinorwe walihisi ni muhimu katika malezi ya watoto. 92% walijibu kuwa jambo muhimu zaidi ilikuwa kuwafunza wanao uwajibifu, 88% walidai kuwa hali ya kujitawala ndilo jambo muhimu (ilihali 11% peke yake walisitiza kuwa watoto wanapaswa kufanya kazi kwa bidii). Ikiwa utafiti kama huu ungefanywa leo, bila shaka ungetoa matokeo yanayokaribiana na haya.

Familia za kigeni ambazo hujifungua katika nchi hii huweza kushuhudia kuwa majirani Wanorwe na marafiki huwapatia nguo za watoto zilizotumika, jambo ambalo wengine wao huonelea ni la kuonyesha nidhamu na kujali, ilihali wengine hukasirishwa kwa sababu wanaogopa kuonekana kama masikini au kuwa Wanorwe wanawaonea huruma. Lakini watoto wadogo hukuwa haraka kabla nguo zao ziwe kuukuu, kwa hivyo Wanorwe huonelea ni jambo zuri kuwa mtu mwengine anaweza kuzitumia. Ni jambo la kawaida kabisa kupatiana nguo kama hizi kwa familia zingine zilizo na watoto wachanga, kwa njia sawa kama ilivyo kawaida kwa Wanorwe kununua vitu vilivyotumika kwenye soko au kwenye maduka ya Fretex yanayosimamiwa na Jeshi La Wokovu.

Maoni kuhusu vijana wa kinorwe ni ya kutofautiana sana. Mwanafunzi mmoja kutoka nchi ya Latvia ametazama kuwa "Msichana halisi wa kinorwe hatumii poda nyingi, anataka kuchomwa na jua kidogo ili awe maji ya kunde, huvalia viatu vya kawaida na hubeba mfuko mgongoni". Watu wengine huhisi kuwa jambo hili halisisitizi usichana wao, na wengine husema ni "uwanaspoti". Maoni kuwa "wasichana wadogo wa kinorwe kwa kawaida huonyesha ngozi nyingi, hunywa pombe na hutembea peke yao usiku wa manane" huchukuliwa kama ishara ya uhuru na pia uasherati. Wasichana kadhaa kutoka familia za kiasia husema kuwa wavulana wa kinorwe ni wapole wanapokosa kuwakodolea macho au kuwapigia mbinja wanapotembea barabarani. Wasichana wengine huhisi kuwa wavulana wa kinorwe ni wakosa nidhamu, kwa sababu hawaonyeshi kupendezwa na washichana. Msichana kutoka familia ya mseto ya kilatvia na kimarekani alifanya ulinganisho ufuatao: "katika nchi ninayotoka, wavulana wanaweza kusema kitu kizuri kama: una kinywa cha kupendeza sana, nywele yako ni nzuri sana, lakini mpenzi wangu wa kinorwe husema tu kitu kizuri juu yangu pale anapendezwa na kile nilichofanya. Anaweza, kwa mfano, kusema kwa njia kavu: "ulifanya jambo hilo vizuri!" pale ambapo nimejiunga na yeye kwa spoti ya kuteleza kwenye theluji kwenye mlima hatari wa kuogofya!"

Kama Wanorwe wengi, wanafunzi wa kigeni hawapendelei kusimama nje na kuvuta sigara kwa aina zote za hali ya anga, lakini haswaa Waasia hufurahia sana kuona kuwa kuvuta sigara kumepigwa marufuku kwa mijengo yote ya umma. Mwindonesia mmoja aliandika kwenye insha kuhusu mada: "Ningependa kumbusu waziri wa serikali aliyeanzisha sheria kuhusu kupigwa marufuku kwa uvutaji wa sigara!" Wengine hushangazwa sana kuwa wasaidizi madukani katika nchi hii huulizia kitambulisho ili wathibitishwe kuwa vijani kweli ni miaka 18 kabla ya kuwauzia sigara au pombe (na kuwa umri halali wa kununua mvinyo na divai ni 18 na 20).

Kama inavyotarajiwa, wakaaji wa kigeni huwa na maoni tofauti kuhusu jinsi Wanorwe hujitaadhabu, kulingana na matarajio yao kwa misingi ya tamaduni zao binafsi. Wengine hutaja kuwa Wanorwe kazini hutabasamu kwa nadra – wengine huandika kuwa Wanorwe hutabasamu sana kazini. Mwanafunzi mmoja kutoka Iraki aliandika kwenye insha kuwa mara ya kwanza kuona afisa wa polisi akitabasamu ilikuwa nchini Norwe. Wanafunzi wengine wa kigeni huonelea kuwa wahadhiri wa kinorwe hufanya vichekesho kupindukia; wao ni watu wenye mamlaka wanaopaswa kuwa wazito zaidi. Wengine huonelea ni jambo zuri sana kuwa wahadhiri au wakurugenzi wa makampuni ni wacheshi na huweza kucheka kazini, na huweza pia kuyakiri makosa yao. Wakaaji wengine wa kigeni huonelea kuwa ni jambo baya sana kuwa wanawake waja wazito bado huenda kazini na hufanya kiwango sawa cha kazi kama hapo awali, na kuwa hawabaki nyumbani kwenye kitanda baada ya kujifungua na kuwa hawana msaidizi nyumbani familia inapompokea mtoto aliyezaliwa. "Wanawake Wanorwe wana nguvu mno, wanaweza kufanya mazoezi na spoti na pia kuvuta makasia walipo waja wazito," aliandika mwanafunzi kutoka India.

Husiano ambazo tunaonelea kama urafiki hutegemea labda tamaduni zetu binafsi. Wanorwe huelezwa kuwa sio rahisi kwa wakaaji wa kigeni kupata marafiki nchini Norwe. Lakini Mwamerikani aliandika mahali fulani kuwa unapofanya urafiki na mtu nchini Norwe, huwa rafiki yako daima, na kuwa rafiki Mnorwe anaweza kutegemewa daima na huweka ahadi.

Wanorwe wengi hawajisumbui na kushikilia mlango kwa wale walio nyuma yao, jambo ambalo lilifafanuliwa kwa roho nzuri na mwanafunzi wa kijeremani: "Kuna watu wachache mno nchini Norwe, na haihitajiki kumshikilia mtu mlango unapotoka nje, kwa sababu mara nyingi hupita dakika tano kabla ya mtu mwengine kupita hapo."

Wakaaji wengi wa kigeni wametazama kuwa Wanorwe halisi hukasirishwa wanapokatizwa katika mazungumzo yao. Pia Wanorwe hawapendelei kusimama karibu sana na mtu wanayemzungumzia, ingawa wanapenda kuangaliana macho kwa macho katika mazungumzo hayo. Kule kuangaliana macho kwa macho kunatafsiriwa kama ishara ya ukweli na kusema yale mtu anahisi. Wengine hawana shaka kuwa Wanorwe ni wabaguzi wa rangi na wazito – wengine huonelea kuwa Wanorwe ni *wapole kupindukia* na wenye kufanya mambo taratibu *kupindukia* inapohusu kutoa maoni kuhusu tamaduni zingine na watu wa nchi tofauti, kuwa wao ni "wapole" sana kwa kiwango kinachofanya liwe jambo gumu kuelewa hisia zao za kweli. Katika mkono mwingine, husemekana kuwa Wanorwe husema mambo moja kwa moja bila ya kusita: "Katika mazungumzo, wanawake na wanaume wa kinorwe wanaweza kutokubaliana vikali, lakini bado hubaki marafiki". Madaktari Wanorwe kwa kawaida hawapigi vijembe, hata inapohusu kuwasiliana kuhusu maradhi hatari. Hawamfichi mgonjwa chochote, na wakaaji wa kigeni kwa kawaida huhisi kuwa jambo hili ni la kinyama.

Ni vigumu kukosa nidhama kwa ”njia sahihi”

Kile ambacho ni onyesho la nidhamu au onyesho la utovu wa nidhamu hutegemea, hata katika utamaduni mmoja, au ndani ya mji mmoja au kijiji. Kuapa kwa kawaida hakukubaliki na huonelewa kama utovu wa nidhamu – na kwa kweli huwa vigumu kutumia maneno ya kuapa kwa njia sawa katika utamaduni mgeni na katika lugha nyingine. (Na kuongezea, maneno hayo yanaweza kutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine). Kusema *dette var jævlig godt (chakula hiki ni kitamu kishenzi)*, ingekuwa utovu wa nidhamu na tamko lisilopendeza mezani, katika karamau ya chakula cha jioni kwa familia, lakini inaweza kuwa njia ya urafiki ya mawasiliano kati ya vijana. Kama mawasiliano yote mengine, hutegemea aina ya uhusiano kati yako na unayemzungumzia, kile mnachozungumzia na muktadha wa mazungumzo yenu.

Wakati mwingine twapata haja ya kutamka kutoridhika kwetu, kukasirika, hasira na kufadhaishwa. Kile unachosema unapokasirika na kile kinacholeta matokeo bora kinategemea utamaduni na yule unayemzungumzia. Kule kutafsiri maneno ya kutukana moja kwa moja kutoka lugha ya mama hutoa nadra matokeo yanayokusudiwa katika lugha nyingine. Chukua, kwa mfano, neno la kiingereza ”bastard”, ambalo ni chaguo bovu ikiwa ungependa kumtukana Mnorwe. ”Bastard” hutumika katika lugha ya kinorwe kumtaja mbwa aliye na wazazi wa aina mbili tofauti. (Neno bora zaidi hapa la kinorwe lingekuwa ”dritt-sekk” – mfuko ambao farasi walibeba chini ya mikia yao kwa kukusanya vinyesi vyao walipotembea barabarani katika siku za kale).

Kisa cha njia isiyo ya kinorwe ya kuonyesha utovu wa nidhamu kilihadithiwa wanafunzi wa kigeni kule Volda: mwanafunzi kutoka nchi ya mbali alitaka kupata leseni ya kuendesha gari nchini Norwe, lakini akaanguka mtihani. Katika hasira na kufadhaishwa kwake kwa kufeli mtihani, alitaka mtahini aliyemwangusha apate kujua jinsi alivyohisi juu yake, kwa hivyo yule mwanamume kutoka ng’ambo akanweleza kitu kibaya zaidi unayoweza kumweleza mtu mwingine katika utamaduni wake: ”Nimefanya mapenzi na dadako!”, pale ambapo mtahini Mnorwe alimwanguka kwa mshangao na kumwuliza kwa utulivu: ”Ahaaa, kweli – wamfahamu?”

”Wageni wenye tabia mbovu”

Kunazo eneo mbili ambapo Wanorwe huwa waangalifu – lugha yao na mandhari. ”Ningependa kujifunza kinorwe cha kweli, sio lahaja,” unaweza kuwasikia wakaaji wa kigeni wakisema, hadi pale ambapo wao hugundua kuwa Wanorwe *wote* huzungumza lahaja, kuwa hakuna lahaja iliyo sahihi kuliko nyingine, na kuwa Wanorwe kwa jumla hujivunia lahaja zao. Hiyo ni kwa sababu lahaja yako ni sehemu muhimu ya utu wako, na huonyesha unakotoka. Katika maeneo mengi, huonelewa kama jambo la aibu mtu anapobadilisha lahaja anapohama kutoka eneo moja la nchi hadi lingine au kutoka jiji moja hadi lingine. Na iwapo mtu atapata elimu ya juu, basi huenda yeye atazungumza zaidi kilahaja – hata wanapohojiwa kwenye runinga, wanapohadhiri kwenye chuo kikuu au wanapozungumza kama wanasiasa. Wasanii wengine wanaotumbuiza huimba na kutunga katika lahaja zao. Hatufurahii mtu anapokosoa lahaja zetu, lakini ni sawa kabisa watu wengine wanapotueleza kuwa hawatuelewi, ili tukarudie tunayoyasema kwa njia nyingine.

Tukizingatia hisia kama hizi kuhusu lahaja, mwandishi wa kitabu hiki aliyekuwa akishuhudia karamu ya chakula cha jioni kule Paris, alikosa nidhamu bila ya kujua, hadi kiwango cha kutoweza kujikosoa (haya yalifanyika muda mrefu uliopita!). kila mtu alikuwa akiendelea na mazungumzo yake kwa utulivu, jambo ambalo lilimaanisha kuwa kila mtu alizungumza *mmoja* baada ya mwingine huku wengine 15 wakisikiliza taratibu. Nilimgeukia mwenzangu

msomi kando yangu na kutoa maoni yangu kwa roho nzuri: "Ahaaa, kumbe unatoka Marseille, singeweza kufahamu hivyo kwa kuisikia lahaja yako." Kulikuwa na kimya kama kaburi pale mezani, hadi pale ambapo mwanamke mpole mfaransa aliposema jambo kuhusu maua yaliyokuwa mezani.

"Una maoni yapi kuhusu Norwe?" ndio swali la kawaida ambalo wageni hupokea, na Wanorwe wanaouliza hutarajia kusikia jambo la sifa kuhusu mandhari ya Norwe. Tunapokosa kupokea jibu "sahihi", sisi hushangaa na labda hufadhaishwa. Ni vigumu kufikiri kuwa kuna watu wasiopendezwa, kama sis tunavyopendezwa, na milima, mito na maunguko. Lakini kwa kawaida itategemea kile utakacholinganisha nacho, na mtazamo utakaochukua. Mwanafunzi kutoka nchi tambarare ya Latvia alisema alipofungua dirisha katika Chuo Kikuu Cha Volda lililoangaliana na milima ya Sunnmøre mbele yake: "Hakuna mandhari hapa. Ninaona milima tu, pote niangaliapo!" Mwanafunzi mmoja Mchina alionelea kuwa ilikuwa jambo la kuogofya kutembea kwenye barabara ndefu bila ya kumwona mtu au nyumba, na katika insha, alitoa utafsiri wake wa tabia ya Wanorwe ya kutembea milimani: "Wanorwe wanapokasirika, hupanda milima." Mgeni kutoka upande mwingine wa dunia alipelekwa kwenye eneo tambarare juu ya mlima ambapo kulikuwa na mandhari nzuri ya milima iliyokuwa na theluji kileleni iliyoonekana hadi mwisho wa kipeo cha macho. Alitazama mara moja na kuuliza: "Kwa nini tuko hapa?"

Kuna msemu maharufu nchini Norwe unaodai kuwa Wanorwe wote huzaliwa na vifaa vya kuteleza kwenye theluji miguuni, lakini huku ni kupindukia. Sio kila mtu anayefahama au aliye na usikilivu wa kushiriki katika spoti za kuteleza kwenye theluji, lakini idadi kubwa ya Wanorwe huvutiwa na maisha ya nje. Hata memba wa familia ya mfalme hawajaachwa nje; kwa vizazi vitatu, wao wamefurahia mazuri ya mazingira, ardhini na majini, na malkia haswaa huchukua safari za siku nyingi milimani kila apatapo nafasi. Mfalme na malkia waliposherehekea miaka 25 ya ndoa, waliwaalika wageni wao waheshimiwa kutoka mbali na karibu kwenye kijibarabara fulani kiliopo katika shamba pweke milimani, inayoangaliana na mto magharibi mwa Norwe.

Miji katika nchi ya Norwe ni midogo, lakini Wanorwe wengi huchagua kuishi nje ya maeneo kama haya. Iwapo watapata kazi, hata Wanorwe wenye ufundi wa hali ya juu huamua kuishi kwenye vijiji vidogo na maeneo madogo. Nafasi nyingi, nyumba bora zaidi kuliko mjini, mahali pazuri pa kulelea watoto na kuishi karibu na mandhari huonelewa kama baraka, haswaa ikiwa una familia. Kupata elimu ya juu sio shida pia, kwa sababu kuna zaidi ya vyuo vikuu 20 vilivyojengwa nje ya miji mikubwa. Tofauti kati ya miji na vijiji tunapozingatia hali ya maisha, njia ya kuishi na tabia ni kidogo sana, ikilinganisha na nchi zingine nyingi. Yawezekana kuwa kwa njia moja au nyingine, wakaaji wa kigeni wanaweza kufurahia zaidi kuishi Norwe kijijini kuliko Norwe mjini, kwa sababu tamaduni fulani ambazo wangependa kupata, bado hutumika kwa viwango tofauti vijijini: watu kwa kawaida huwafahamu majirani wao, mtu huwatembelea marafiki na majirani mara kwa mara bila ya mwaliko, na haswaa watu wakongwe watazungumza na wageni na kuwauliza majina yao, wanakotoka, wazazi na wazazi wa wazazi wao ni nani – na haswaa vijana hukasirika wanapopokea maswali mengi kama haya.

Si wakaaji wote wa kigeni waliosafiri sana nchini Norwe, lakini wakati mwingine unaweza kupata hisia kutokana na jinsi wanavyoandika na yale wanayoyasema, kuwa wana hisia mbaya kuhusu maeneo ya vijijini, huku wakidai kuwa wakulima na watu waishio vijijini ni wapumbavu, washamba na wasiojua mengi. Ikiwa unataka kufanya urafiki na Mnorwe, *Usiwahi* kuanza mazungumzo kwa kutoa maoni yako kuhusu lahaja ya mtu usiyoipenda au

kwa kuuliza: "Yaweze kana kweli kuishi mahali kama hapa? Hakuna mtu hapa, na hakuna chochote cha kufanya."

Imetajwa hapo awali kuwa wakaaji wengi wa kigeni na watalii huonelea kuwa Wanorwe ni wanyamavu na wasio na haja na watu, wanapokosa kuzungumza na watu wasiowajua kwenye basi au gari la moshi. Kwa upande wao, Wanorwe wengi huhisi kuwa wakaaji wa kigeni na watalii ni wakosa nidhamu kwa kutowaacha watu wakae kwa amani. Baada ya siku ndefu kazini mtu huwa mchovu, na kwenye basi mtu anaweza kuketi na kupumzika. "Je, ni jambo la nidhamu na la kirafiki kweli kuwa na mazungumzo ya juujuu na mtu usiyemjua na ambaye hautawahi kukutana naye tena?" ni swali ambalo Wanorwe kadhaa wanaweza kuuliza. Wanorwe wenyewe wanapotembelea nchi zingine kama watalii, lakini, hutaka kuzungumza na "wenyeji", na kwa kawaida hupiga soga kwenye basi au gari la moshi.

Wanorwe wanaweza kukasirishwa na wakaaji wa kigeni wanaozungumza kwa sauti ya juu kwenye basi au kwenye duka, wanakaribia kupigiana mayowe, huku wakaaji wa kigeni wakionelea kuwa sio jambo zuri kuwa Wanorwe ni "watu wanyamavu". Mkaaji wa kigeni alisema katika mahojiano kwenye runinga kuwa "Wanorwe hutokubaliana kirahisi kwa matamshi na watu wengine kazini na katika maisha yao binafsi, lakini hawawezi kuonyesha kuwa wamekasirika. Yakaribia kuwa jambo la kuogofya kuwa wao huwa watulivu wakati wote. Ninatamani kuwa mara moja ningewaona Wanorwe wawili wazima wakipigana na kutukanana barabarani".

Kitu kimoja ambacho huwakasirisha sana watalii wa kinorwe katika nchi zingine ni jinsi ambavyo wauzaji barabarani, sokoni na madukani huwa na hamu sana ya kuwauzia bidhaa zao. Muuzaji anaweza kukufuata na kukasirika sana ikiwa amekuonyesha bidhaa zake bila ya wewe kununua chochote. Ni tofauti nchini Norwe, ili wakaaji wa kigeni na watalii katika nchi hii wasidhani kuwa wasaidizi madukani ni wavivu na wasiotaka kutoa huduma zao, wanapomwacha mteja azunguke na kutazama bidhaa bila ya kutoa usaidiza wao mara moja. Sababu yaweza kuwa eti Wanorwe hupendelea kudadisi bidhaa bila ya kusumbuliwa, huku pia tukitarajia msaidizi dukani atuonyeshe aina zingine za bidhaa bila ya kumaanisha kuwa ni lazima tununue chochote.

Unapohamia nchi mpya, watu wanaweza kuhisi kwa urahisi kuwa unakosa nidhamu kwa sababu hauzifahamu kanuni za kujitaadhabu. Wakaaji wengine wa kigeni hujaribu kupatana bei juu ya kile wanachotarajia kulipa sokoni au dukani katika nchi hii, kama walivyozea kufanya katika nchi zao. Huku, jambo hili laonelewa kuwa utovu wa nidhamu, kwa sababu bei hazibadilishwi na hakuna utamaduni wa kupatana bei katika nchi ya Norwe isipokuwa kwenye soko la kuuza vitu vilivyotumika, hata ingawa ilikuwa kawaida hapo zamani, kwa mfano, uliponunua na kuuza farasi. Unapojaribu kupatana bei kwenye duka, wasaidizi wa kinorwe kule dukani watahisi kuwa unawashuku kwa kujaribu kumtoza mnunuzi pesa nyingi kupindukia.

Kitu kimoja ambacho nimeshuhudia katika miaka yangu 17 ya kufanya kazi na wanafunzi wa kigeni kutoka nchi 77 tofauti, ni kuwa wao huwasiliana kwa nadra ikiwa habari walio nayo ni mbaya. Jambo hili linaweza kuleta kufadhaika, kwa sababu Wanorwe wapole watakujulisha ikiwa hawataweza kufika kwa wakati ufaao kwa mwaliko au mkutano, na kama hawawezi kutenda jambo kwa wakati uliokuwa umeahidiwa.

